

**Tuzo** za Oscar zasogezwa mbele

UKURASA 20



**Lingard** yupo tayari kurudi West Ham

UKURASA 21

**MAISHA** Jumapili

Mei 30, 2021 Nipashe

Baba, Mama na Mwana






Mzazi ni daraja la mtoto kutimiza ndoto yake

MAISHA NI NYUMBA

Namna ya kufanya meza yako ya chakula kupendeza



HARUSI



'HEELS'

Raha, karaha za viatu virefu

UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Mei 30, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580596

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# CHADEMA wampa wiki 3 Spika Ndugai

• **Wadai** wanajipanga kumshangaza... *Endelea ukurasa 2*



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe, akiweka jiwe la msingi kuzindua ujenzi wa Ofisi ya chama hicho, Jimbo la Shinyanga Mjini, eneo la Ndala, Manispaa ya Shinyanga, jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

## YALIYOMO




UKURASA WA 2
MAWAZIRI TANZANIA, KENYA WAKUTANA VIKWAZO BIASHARA

UKURASA WA 4
JAFO ATAKA KILA HALMASHAURI MITI MIL. 1.5 IPANDWE


## Mwinyi abanwa kuosha vyungu

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store




## Serikali yaagiza msako wahalifu miezi mitatu

UKURASA 2


**MICHEZO** AZAM YAIWEKA KANDO SIMBA, AKILI LIGI KUU UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Serikali yaagiza msako wahalifu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KUFUATIA kushamiri kwa vitendo vya uhalifu nchini, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, ameagiza Jeshi la Polisi mikoa yote kufanya msako wa wahalifu kwa miezi mitatu mfululizo ili kukomesha vitendo hivyo.

Pia, ameagiza kutoachiwa kwa mahabusu wanaokamatwa hadi watakapofikishwa mahakamani hata kama kutakuwa na msongamano maeneo ya kuwahifadhi.

Simbachawene alitoa maagizo hayo jana alipozuru katika Kituo Kikuu cha Polisi Mkoa wa Dodoma na kushuhudia watuhumiwa waliokamatwa kwenye operesheni maalum ya kudhibiti uhalifu inayoendelea mikoa yote.

Alisema uhalifu hauna nafasi Tanzania na msako huo unaendelea kwenye mikoa yote na hakuna kusimama kwa miezi mitatu.

"Matukio ya kukaba, kubaka, kuvunja nyumba, kuiba simu, runinga, kunyang'anya mikoba ya kinadada kwa kutumia bodaboda, yamekuwa mengi sana.

"Na ni kundi hili la vijana hawataki kufanya kazi halali, wanataka kujihusisha na uhalifu.

"Ninampongeza RPC (Kamanda wa Polisi Mkoa) Dodoma, hii ni kazi nzuri kwa siku mbili tu kundi hili kubwa, tutatafuta magereza, tutatafuta pa kuwaweka, masuala ya kusema msongamano, msongamano watu tunawaachia wanaenda mtaani wanaendelea kutuumiza," alisisitiza.

Alisema watuhumiwa wa uhalifu watahifadhiwa popote na polisi na watalindwa na bunduki hata kama mahabusu zimejaa.

"Tutawaweka hapa na kuwalinda hapa hapa, hadi wapelekwe mahakamani na wengine wakafungwe.

"Kwa mfano, Dar es Salaam kila wanaokamatwa kwenye msako lazima wawili au watatu wawe ni waliopata msamaha wa kutoka gerezani," alisema.

Simbachawene alisema Tanzania ni nchi ya amani na watu wanatakiwa kufanya shughuli zao bila kubughudhiwa.

"Watu wanashindwa kulaza TV zao sebuleni hadi wanalala nazo vyumbani kwa sababu yenu na wizi wa simu, Jeshi la Polisi endeleeni, moto ni huu huu, ninaamini jeshi lipo imara, lina watu wazoefu, kamateni wote wapelekwe mahakamani," aliagiza.

Alitaja sababu ya kutowapa dhamana mahabusu kuwa wengi wanaoachiwa wamekuwa wakirudia kufanya makosa hayo hayo.

Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, Gilles Muroto, alisema wamekamatwa watuhumiwa 60 wa uhalifu kwa siku mbili, wakiwamo wanaodaiwa kupora kwa kutumia bodaboda.

# CHADEMA wampa wiki tatu Ndugai

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BARAZA la Wanawake la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), limetoa siku 21 kwa Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuwafukuza bungeni wabunge 19 wa viti maalum wanaotokana na CHADEMA kwa kuwa wameshafutiwa uanachama.

Katibu Mkuu wa Baraza hilo, Catherine Ruge, alitoa tamko hilo jana mkoani Shinyanga wakati Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, alipozuru mkoani hapa kwa lengo la kukiimarisha chama hicho.

Catherine alisema baraza hilo limejipanga vyema kumshangaza Spika Ndugai endapo akishindwa kuwafukuza bungeni wabunge hao, wakiongozwa na aliyekuwa Mwenyekiti wa BAWACHA, Halima Mdee.

"Spika Job Ndugai asidhani BAWACHA tupo kimya juu ya kuendelea kuwalinda kina Halima Mdee na wenzake, tunampa siku 21 awe ameshawafukuza bungeni, tofauti na hapo tutamshangaza.

"Pia, sisi BAWACHA bila ya kuwapo tume huru ya uchaguzi, hatutashiriki kwenye uchaguzi ujao wa serikali za mitaa mwaka 2024 pamoja na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kwa sababu hatutakubali kuporwa tena ushindi," alisema.

Spika Ndugai amekuwa akisisitiza kuwa ameshindwa kuchukua uamuzi wa kuwafukuza bungeni wabunge hao kutokana na kutokujitosheleza kwa barua aliyoipokea kutoka kwa Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, kuhusu suala hilo.

Katika ziara yake hiyo mkoani Shinyanga, Mbowe alionya usaliti ndani ya chama hicho na kubainisha kuwa yule ambaye atakwenda kinyume cha katiba yao watamfukuza kama walivyofanya kwa kina Mdee.

Mbowe pia alitumia fursa hiyo kutaka uandikishaji mpya wa wapigakura kwenye daftari la kudumu la mpigakura huku akitaka kuchukuliwa hatua kwa maofisa wote wa tume waliobainika kufanya kile alichokiita kuharibu uchaguzi.

Pia, alisisitiza kutoipokea ruzuku ya serikali kwa ajili ya kuendesha chama hicho kwa kuwa wako tayari kupambana wenyewe kutafuta fedha na ndio maana wamezindua mkakati wa CHADEMA Digital ili wapate fedha kupitia wanachama.

Mbowe alisema watakwenda kufanya utafiti wazo la kupiga kura kwa njia ya mtandao kwenye uchaguzi ujao, ili kusiwapo alichokiita wizi wa kura wala kununuliwa kwa mawakala.

Katika ziara hiyo, Mbowe alifuatana na Naibu Katibu Mkuu CHADEMA Zanzibar, Salumu Mwalimu, Naibu Katibu Mkuu CHADEMA Tanzania Bara, Benson Kigaila na Kaimu Mwenyekiti wa BAWACHA, Sharifa Suleiman.



Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Thobias Mwilapwa (kulia), akikabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Pangani, Toba Huvila, katika Kijiji cha Kimang'a, kwa ajili ya kuanza kukimbizwa wilayani humo jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mawaziri wakutana vikwazo vya biashara Tanzania, Kenya

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MKUTANO wa mawaziri wa Kenya na Tanzania unaendelea jijini Arusha, miongoni mwa agenda kuu ikiwa ni kujadili na kutatua vikwazo vya biashara visivyokuwa vya kiushuru.

Hatua hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa maazimio yaliyofikiwa na wakuu wa nchi hizo mbili wakati wa ziara ya kiserikali ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini Kenya Mei 4-5 mwaka huu.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, jijini Arusha jana, alibainisha kuwapo kwa majadiliano hayo. Alisema kuwa katika ziara ya Rais Samia nchini Kenya, pamoja na mambo mengine, wakuu wa nchi waliwahakikishia wafanyabiashara wa Tanzania na Kenya kuwa serikali za nchi zote mbili ziko tayari kuwapa ushirikiano wowote watakaouhitaji na kuweka mazingira mazuri ya kukuza biashara na uwekezaji katika nchi zote mbili.

Kwa mujibu wa Waziri Mkenda, mahitaji ya mahindi Kenya ni takriban tani 600,000, hivyo vikwazo vilivyopo katika mipaka ya Holili na Namanga havina tija kwa nchi zote mbili kwa kuwa Tanzania inalihitaji soko la Kenya kwa ajili ya mazao ya wakulima wake na Kenya ina uhitaji na mazao mbalimbali hususani mahindi kutoka Tanzania. Alisema mkutano huo pamoja na kujadili kuhusu vikwazo vya biashara visivyokuwa vya kiushuru, pia utatoa fursa ya kujadiliana na kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu biashara ya mazao na bidhaa zinazotokana na mazao.

"Tunakwenda katika mkutano huu tukiwa na agenda ya kuhakikisha kuwa tunaendelea kumkwamua mkulima wa Tanzania katika kutafuta masoko ya mazao kwenda Kenya, vilevile ya Kenya kuja nchini," alisema.

Hivi karibuni, wafanyabiashara wa mahindi wanaonunua mahindi nchini na kuyasafirisha kwenda Kenya, walibainisha kupata hasara kutokana na uamuzi wa Serikali ya Kenya kuzuia majindi ya Tanzania kuingia nchini mwake.

# Mwinyi alivyobanwa kuosha vyungu alfajiri

**Na Christina Mwakangale**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amebainisha kuwa ilimlazimu kuwa anaamka mapema asubuhi kufanya kazi za nyumbani, ikiwamo kuosha vyombo kabla ya kwenda shuleni.

Amesema ratiba hiyo ya kila siku haikuishia hapo, bali ilimpasa pia kufagia uwanja nje na ndani ya nyumba waliyokuwa wakiishi pamoja na kuchota maji kwa ajili ya kufanyia usafi.

Mwinyi anasimulia hayo kwenye kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', kilichozinduliwa mwezi huu.

Anasema hayo yalijiri wakati akiishi Mangapwani, Unguja kwa Mzee Suwedi Bin Mgeni, rafiki wa baba yake, Mzee Hassan, alipokwenda kwa ajili ya kusoma shule.

Anasema baba yake (marehemu) alikusudia mwanawe asome elimu akhera hadi chuo kikuu ndiyo sababu aliamua kumpeleka kuishi Unguja na familia ya Mzee Suwedi.

"Nilijikuta Januari 5 mwaka 1933 nimo katika darasa la kwanza, baada ya mlezi wangu Mzee Suwedi, kunipeleka Shule ya Mangapwani kuanza masomo.

"Nyumbani mwetu (kwa Mzee Suwedi), hakukuwapo mtoto mwanamke, tulikuwamo watatu, wote wanaume. Wakati nilipoanza shule nilikuwa na miaka minane na nusu.

"Waswahili wanasema 'lisilo budi hufanywa'. Mama mwenye nyumba ameamuru kumsaidia kazi za nyumbani... kwa mvulana kuishi katika nyumba isiyokuwa na msichana, hapana budi kutoa msaada unaohitajika kuendesha nyumba.

"Kwa kuwa chakula cha usiku kilikuwa kinaliwa saa tatu za usiku, vyungu na sufuria zinazopikiwa chakula ingebidi vioshwe asubuhi kesho yake kabla sijaenda shule. Kila kukicha nilienda jikoni kuvikusanya," anasimulia.

Mwinyi anasema kutokana na vyungu hivyo kuwa vikubwa na kumzidi kimo chake, alilazimika kuvikumbatia wakati akivibeba kuhofia visivunjike hadi sehemu ya kuoshea vyombo.

"...ilinilazimu kuvikumbatia ili kuhakikisha haviniponyoki na kuvunjika maana ingekuwa balaa kubwa... matokeo ya kupakata vyungu ilikuwa kujieneza masizi, nguoni na mwilini, nilipokwenda shule saa moja na nusu asubuhi huwa mchafu," anasimulia.

Mwinyi anasema kwa kipindi hicho miaka ya 1930, kama zilivyokuwa nyumba nyingine ambazo hali ya umaskini ilishuhudiwa, watoto wengi kununuliwa nguo ilikuwa ni mara moja kwa mwaka hasa msimu wa sikukuu.

"Shule yetu ilikuwa kati ya bahari mbili. Hivyo, kusafisha nguo zangu wala kukoga, hayakuwa mambo magumu, siku ya Jumapili, Ijumaa watoto tulishinda pwani tukifua nguo, kuogelea kutwa.

"Tukitoka kwenye maji huwa nguo zetu za 'kauka nikuvae' zimekauka tunazivaa kisha tunatawanyika," anasema.

Katika kitabu hicho, mbali na masuala muhimu ya kitaifa, kinanda na kimataifa, Mwinyi anasimulia kwa kina historia ya maisha yake ya takribani miongo tisa.




Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Angelina Ngalula (wa pili kushoto), akifungua mkutano wa mwezi wa Chama cha Wafanyabiashara Wanawake (TWCC), jijini Dar es Salaam jana. Kushoto Mwenyekiti mstaafu wa chama hicho, Jacqueline Maleko, Mwenyekiti wa Bodi ya TWCC, Mercy Sila (katikati), Mkurugenzi Mtendaji wa chama hicho, Mwajuma Hamza (kulia) na Mjumbe wa Bodi, Rose Romanus. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri aonya TANESCO kupokea kazi za vishoka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ameliagiza Shirika la Umeme (TANESCO) kuhakikisha linapokea kazi za mafundi umeme waliosajiliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (EWURA) ili kudhibiti vishoka.

Alitoa agizo hilo jana alipofungua mafunzo kwa mafundi umeme kuhusu Sheria ya Umeme ya Mwaka 2008 na kanuni za ufungaji umeme za mwaka 2019 iliyoandaliwa na EWURA jijini hapa.

Alisema hatua hiyo itasaidia kupunguza athari za ajali zinazotokana na mifumo isiyo mizuri ya uunganishaji wa umeme kwa wateja.

"Ninaagiza TANESCO kutumia kanzi data ya EWURA katika kupokea kazi za kandarasi za umeme na fundi yeyote mwenye leseni ya EWURA ana uhuru wa kufanya kazi popote Tanzania Bara," alisema.

Vilevile, alizitaka taasisi za serikali na watu binafsi kutumia mafundi ambao wamesajiliwa na wana leseni ili kuepukana na vishoka.

"Tatizo lililopo mafundi wengi wasiosajiliwa wanafanya kazi bila usimamizi, wengine hawana leseni za EWURA na wengine wanatumia leseni mfu ambazo hawajazihuisha hadi leo," alisema.

Waziri huyo alisema umeme ni salama lakini ni hatari.

"Mwenye nyumba anakutegemea wewe, amejenga nyumba kwa Sh. milioni 200, wewe unamfungia umeme lakini umefunga vibaya, nyumba nzima inaungua, hakikisheni kazi zenu zinakuwa salama kwa wateja wenu," aliagiza.

Kuhusu utozaji bei holela za uunganishaji umeme, Dk. Kalemani aliitaka EWURA na taasisi zinazohusika kufanya uchambuzi wa bei halali za mafundi umeme majumbani.

Alisema kuwa suala hilo kwa sasa halina kanuni ndiyo maana kumekuwapo na utozaji bei hizo kiholela na kero kwa wateja.

"Hawajui wanachokilipia ni nini, ni wiring au muhuri? Vijijini lugha inayotembea sana vijijini ni muhuri, kwa hiyo analipia wiring na muhuri, kana kwamba hizo ni kazi mbili tofauti, kinachopaswa kulipiwa ni ufundi wako wa kumuwekea nyaya mteja siyo muhuri, muhuri unakutambulisha wewe," alisema.

Dk. Kalemani alisema kuna tabia anayefanya uunganishaji umeme ni mtu mwingine lakini anayegonga muhuri ni mwingine.

"Kuanzia sasa tunataka aliyefanya kazi hiyo huyo huyo ndiyo agonge muhuri maana unamtambulisha yeye," alisema.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Godfrey Chibulunje, alisema tatizo lililopo sasa mafundi wengi wa umeme wanafanya kazi bila kuwa na leseni na ni kinyume cha sheria ya umeme.

"Kuna mafundi wengi wasiosajiliwa na wanafanya kazi bila usimamizi na hivyo kazi nyingi zinafanywa chini ya viwango na pengine kusababisha ajali za moto muda mfupi baada ya kukamilika," alisema.



# Majaliwa kusikiliza vikwazo Ushirika

**Na Faustine Feliciane**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika kilele cha maadhimisho ya Ushirika Duniani ambapo kwa Tanzania maadhimisho hayo yanafanyika mkoani Tabora kuanzia Juni 23 hadi Julai 3 mwaka huu.

Katika kilele cha maadhimisho hayo, wanaushirika wanatarajiwa kutoa kero na mahitaji yao kwa serikali juu ya ushirika nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mtendaji Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC), Florian Haule, alisema ilivyo kwa maadhimisho ya mwaka 2018, wanatarajia kumwalika Majaliwa ili kufukisha malengo yao kwa serikali. "Kutakuwa na mambo mengi kutoka kwa wanaushirika, tunatarajia Waziri Mkuu kuwa mgeni rasmi pale Tabora katika viwanja vya Nanenane.

"Baadhi ya mambo yatakayokafanyika kwenye maadhimisho hayo ni pamoja na maonyesho ya wanaushirika, kufanya mambo ya kijamii ikiwa ni pamoja na kuchangia damu, kuhamasisha utunzaji wa mazingira na mambo mengine," alisema.

Haule alisema kuwa kaulimbiu ya mwaka huu ni "Ushirika Tujijenge Upya kwa Ubora na Tija'.

"Kaulimbiu hii imekuja hasa kutokana na ukweli kuwa dunia ilipitia changamoto ya corona ambayo pia haikuuacha salama Ushirika, hivyo sasa tumeona tusimame na tujijenge upya na hii ndiyo itakuwa kauli biu yetu ya maadhimisho haya ya 20 ya Ushirika tangu tumeanza kuadhimisha mwaka 2002 hapa Tanzania," alisema.

Aliongeza kuwa katika maadhimisho ya mwaka huu watazindua tuzo maalum kwa viongozi ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa kuinua Ushirika na kuufikisha hapa ulipo sasa.

Alisema Ushirika wana mambo mengi ambayo wanataka kufikisha ujumbe kwa serikali kwa maendeleo ya nchi.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, akipanda mti katika eneo la Medeli, katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# Jafo: Kila halmashauri ipande miti milioni 1.5

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, ameagiza kila halmashauri kuhakikisha inapanda miti milioni 1.5 kila mwaka na kuitunza ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Vilevile, amesema mikoa, vyuo, shule za sekondari na msingi za umma na binafsi zitashindanishwa katika utunzaji wa mazingira na shule au chuo kitakachoongoza kitapewa zawadi ya gari.

Jafo alitoa agizo hilo jana kwenye upandaji miti eneo la Medeli jijini hapa.

Waziri Jafo alisema suala la utunzaji wa mazingira ni shirikishi na linapaswa kufanywa na wananchi wote.

"Miti hii tunayopanda itatusaidia katika suala zima la uharibifu wa mazingira.

"Uharibifu wa ukataji miti ni mkubwa, kila mwaka miti zaidi ya milioni 48 inakatwa, hivyo tuna kila sababu ya kupanda miti.

"Katika ajenda ya upandaji wa miti ninatamani sana kila mwanafunzi wa shule ya msingi awe na miti miwili ama mitatu na kuitunza, suala la upandaji wa miti lishuke hadi ngazi ya familia.

"Kuna maeneo mengine leo hii yamekuwa kame, yamekuwa nusu jangwa kutokana na uharibifu wa mazingira," alisema.

Aliwataka wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri kusimamia upandaji wa miti katika maeneo yao.

"Maelekezo ya Ilani ya CCM, sera zetu za nchi na mipango yetu ya taifa imetuelekeza ni jinsi gani sasa tunatakiwa kuhakikisha tunalinda mazingira yetu.

"Ninazielekeza kila halmashauri lazima zipande miti takribani milioni 1.5 kila mwaka," alisema.

Jafo alisema wameamua mwaka huu kuanzisha kampeni kabambe ya mazingira.

"Tunataka Tanzania Kama nchi iwe ya mfano duniani na ndiyo maana tumeanzisha kampeni hii itakayozinduliwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alimhakikishia waziri huyo kuwa viongozi wa Mkoa wa Dodoma watahakikisha wanatekeleza maelekezo yaliyotolewa.

Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alisema Dodoma unahitaji kupandwa miti na kuahidi kushirikiana na serikali kuufanya mkoa huo kuwa wa kijani.

# TARI yatoa mbegu mpya ya mchicha ya muda mfupi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (TARI) imetoa mbegu mpya tatu za mchicha ambazo zinastawi kwa muda mfupi, hazishambuliwi na magonjwa na zinaimarisha afya za walaji.

Imesema mbegu hizo pia zina protini zaidi ya nyama kwa asilimia 15.

Mratibu wa mradi wa mchicha wa kushangaza, Emmanuel Laswai, kutoka Kituo TARI Tengeru, alibainisha hayo jana jijini Dodoma kwenye jukwaa la wadau wa kilimo cha mchicha mkoani hapa.

Alisema mchicha huo unastawi kwa siku 21 na unavunwa kwa miezi mitatu na kuwataka Watanzania kuchangamkia fursa hiyo ya mbegu zilizofanyiwa utafiti ili kujikwamua kiuchumi.

Laswai alisema mradi huo wa mchicha wa kushangaza unatekelezwa katika maeneo mbalimbali kupitia kanda zake zote na unafadhiliwa na Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika la GIZ.

"Mbegu hizo za mchicha ambazo zimefanyiwa utafiti na kituo cha TARI Tengeru, ni Akeri, Nguruma na Pori, zitawezesha wakulima kujikwamua kiuchumi na kuimarisha afya za walaji kutoka na kusheheni madini mbalimbali pamoja na protini kwa kiasi cha zaidi ya asilimia 15 kushinda hata kiasi cha protini kilichopo kwenye nyama.

"Siyo lazima kuendesha bodaboda, vijana walioko mtaani wanaweza kutumia kilimo hiki kujipatia kipato kwa muda mfupi kwa kuwa sifa zingine zilizopo katika mchicha huu ni kutosumbuliwa na magonjwa," alisifu.

Mratibu huyo aliongeza kuwa mchicha huo ni muhimu kwa matumizi ya lishe ya watoto wadogo kutokana na kuwa na uwezo mkubwa wa kuimarisha afya zao.

"Ili kuondokana na tatizo la udumavu nchini mchicha huu utakuwa msaada mkubwa kutokana na kuwa na madini mengi pamoja na protini muhimu katika ukuaji wa afya za watoto," alisema Laswai.

Alisema kuwa katika aina hizo tatu za mchicha pia upo mchicha nafaka ambao unaweza kutengenezwa unga wa uji pamoja na vitafunywa aina mbalimbali.

Meneja wa TARI Tengeru, Dk. Mpoki Shimwela, alisema lengo la jukwaa hilo ni kuwezesha wakulima kupata teknolojia mbalimbali zinazofanyiwa utafiti katika kilimo cha mchicha.

"Tumekuwa na majukwaa kama haya katika kanda tano za TARI nchini, lengo ni kuhamasisha wakulima kutumia mbegu hizi za mchicha ili kujikwamua kiuchumi lakini pia kuimarisha afya za watumiaji," alisema Dk. Shimwela.

Alisema ili kusaidia kupatikana kwa soko la uhakika wa kilimo hicho, wanaiomba serikali kutengeneza sheria ndogo ambazo zitalazimisha watengenezaji wa unga wa lishe wa watoto kutumia mchicha huo kuongeza virutubisho lishe.

"Wenzetu Kenya tunasikia kuwa wameweka sheria ambayo inataka watengenezaji wa unga wa lishe wa watoto kuwa ni lazima uchanganywe na unga wa mchicha kutoka na kuwa na protini kwa kiasi kikubwa ianayohitajika kwa afya ya ukuaji wa watoto," alisema Dk. Shimwela.

Alisema sheria hiyo hiyo itasaidia kuimarisha na kulinda afya ya watoto pamoja na kuondokana na tatizo la udumavu na watoto wasiofundishika darasani.

HABARI KITAIFA

# Waona shida sheria maendeleo biashara

Na Mwandishi Wetu

CHAMA cha Mawakala wa Forodha Tanzania (TAFFA) kimeshauri sheria zifanyiwe marekebisho kurahisisha ufanyaji biashara na kusaidia bidhaa zinazoingia nchini kuwa na viwango ili kutoathiri wananchi.

Katibu Mkuu Mtendaji wa TAFFA, Elitunu Mallamia, alitoa rai hiyo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kwenye mkutano ulioandaliwa na Shirika la Viwango (TBS) kwa lengo ya kuzipatia ufumbuzi kero mbalimbali wanazokutana nazo kwenye utendaji kazi wao.

"Pale ambapo taarifa zinakuwa zinapatikana kirahisi maana yake mwagizaji ataweza kufuata sheria vizuri na sisi tutaweza kumwelekeza ili kwenda kule ambapo kuna bidhaa zenye viwango ambazo haziwezi kuathiri wananchi wa Tanzania.

"Kwa hiyo tutumie mkutano huo kwa ajili ya kutoa mapendekezo ambayo yatasaidia chama chetu, wanachama wetu na taasisi zingine tunazoshirikiana nazo kuondosha mizigo bandarini.

"Hiyo itasaidia kuhakikisha mizigo inaondoshwa kwenye vituo vyetu vya forodha kwa wakati na nchi inapata mafufaa ya uwapo wa TBS na kibiashara," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Masoko wa TBS, Gladness Kasema, alitoa wito kwa wadau mbalimbali kutosita kuhudhuria vikao kazi kama hivyo kwa kuwa ni fursa muhimu ya kutatua kero walizonazo na hatimaye kuwawezesha kutoa huduma kwa ufanisi.

Alisema tangu wameanza kufanya vikao hivyo na wadau wakiwamo wazalishaji wa bidhaa za aina mbalimbali, tija imekuwa ni kubwa, kwa kuwa malalamiko yamepungua kwa kiasi kikubwa.

Kaimu Mkurugenzi Udhibiti Ubora, Moses Mbambe, alisema lengo la mkutano huo na TAFFA ni kuboresha utaratibu wa ufanyaji kazi wao hasa kwa kuzingatia kuwa mizigo inayoingia nchini inakidhi matakwa ya viwango vya ubora na usalama.

"Kwa hiyo wakati wa uingizaji mizigo kwa ajili ya wateja wao ni lazima zihakikishwe zinakidhi utaratibu wa uagizaji mizigo za shirika letu," alisema Mbabe.

Alisema kupitia kikao kazi hicho wameamua kukumbushana taratibu za shirika kwa lengo la kukumbushana ubora na usalama wa bidhaa.

# Mfumo mpya kutumika uhamisho wa watumishi

**Na Mwandishi Wetu,**
SUMBAWANGA

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Dk. Laurean Ndumbaro, amesema kuanzia Julai, mwaka huu mfumo mpya wa Kitanzania wa taarifa za kiutumishi na mishahara utatumika kuchakata na kuoanisha maombi ya vibali vya uhamisho wa watumishi wa umma.

Amesema kuanza kutumika kwa mfumo huo kutapunguza malalamiko ya watumishi kuhusu kero iliyopo ya upatikanaji wa vibali vya uhamisho kuchukua muda mrefu.

Dk. Ndumbaro aliyasema hayo mjini Sumbawanga juzi alipozungumza na watumishi mkoani Rukwa wakati wa ziara yake ya kikazi yenye lengo la kuhimiza uwajibikaji na kutatua kero zinazowakabili watumishi wa umma mkoani humo.

Alisema mfumo huo utakapoanza kufanya kazi, utaboresha ufanisi wa waajiri katika kuratibu zoezi zima la uhamisho wa watumishi wa umma nchini.

"Baada ya watumishi kuomba uhamisho, maombi yote yataingizwa kwenye mfumo ambapo yatachakatwa, kuoanishwa na kuwasilisha kwenye mamlaka husika kwa ajili ya kutoa kibali," Dk. Ndumbaro alifafanua.

Alisema kuwa ili kuhakikisha uhamisho hauibui tatizo la uhaba wa watumishi kwenye maeneo ya uhitaji mkubwa wa rasilimaliwatu, wakuu wa taasisi za umma, wakurugenzi watendaji, makatibu tawala mkoa, Katibu Mkuu TAMISEMI na Katibu Mkuu Utumishi wamepewa uwezo wa kuona na kuratibu maombi yote ya uhamisho ndani ya maeneo yao ya utawala.

Alisema kwa msingi huo, suala la uhamisho litakuwa rahisi kufanyiwa kazi na mamlaka, hivyo watumishi wataruhusiwa kuhama pasi na vikwazo visivyo na msingi wowote.

Mtumishi Kilingo ambaye ni mwalimu, aliipongeza serikali kwa kuunda mfumo utakaoratibu uhamisho na malipo ya madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi (automatic) na kuongeza kuwa mfumo huo utapunguza kero zilizokuwa zikiwakabili watumishi wa umma nchini kwa kipindi kirefu.

Mwalimu Kilingo pia alimpongeza Dk. Ndumbaro kwa kuupa Mkoa wa Rukwa ofisa anayeshughulika na mfumo anayewajibika kikamilifu tofauti na aliyekuwapo mwanzo ambaye alilalamikiwa kwa kutotekeleza majukumu yake kwa wakati.

Dk. Ndumbaro alihitimisha ziara ya kikazi ya siku mbili mkoani Rukwa na kwenda mkoani Katavi kuendelea na ziara yake yenye lengo la kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi waliopo katika mkoa huo.

# Wizara yatoa elimu kodi ya ardhi nyumba kwa nyumba

**Na Halfani Chusi**

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeendelea na utoaji wa elimu nyumba kwa nyumba kuhamasisha wamiliki wa ardhi kutambua umuhimu wa kulipa kodi ya ardhi.

Juzi, elimu hiyo ilitolewa mkoani Dar es Salaam na Ofisa Ardhi Kanda ya Dar es Salaam, Ramla Mwasha, aliyeongozana na jopo la moofisa ardhi na waandishi wa habari maeneo ya Mbagala Kijichi.

Ofisa huyo alisema kuwa baadhi ya wananchi walikuwa wanashindwa kutofautisha kati ya kodi ya ardhi na kodi ya majengo.

Alisema hali hiyo inasababisha kikwazo kikubwa kwa baadhi ya maofsa ardhi wakati walipopita mitaani kukusanya kodi kwenye baadhi ya maeneo.

"Kulikuwa na changamoto kubwa sana ndiyo maana tumeamua kutoa elimu hii nyumba kwa nyumba ili kuwaongezea wananchi uelewa juu ya suala zima la kodi ya ardhi na majengo.

"Tuligundua kuna baadhi ya wananchi hawana uelewa wa kutosha juu ya kodi ya ardhi na kodi ya majengo," alisema.

Alifafanua kuwa kodi ya ardhi ni anayolipia mmiliki wa kiwanja ambacho kimepimwa na wizara na kutambulika kiserikali na kodi ya jengo ni anayolipia jengo lake hata kama limejengwa sehemu isiyopimwa na wizara na kuongeza kuwa kodi hiyo inalipwa mara moja kwa mwaka.

Ofisa huyo alisema tangu kuanza kutolewa kwa elimu hiyo, wamefanikiwa kukusanya Sh. bilioni 34 kati ya bilioni 69 walizokuwa wamepanga kukusanya ndani ya mwaka mmoja.

Mwajuma Bakari, mkazi wa eneo hilo, alikiri kunufaika na elimu hiyo na kusisitiza imempa ufahamu mkubwa, akiiomba wizara kufanya suala hilo kuwa endelevu.

"Leo nimepata kitu kipya kichwani mwangu, nimegundua kuwa kiwanja changu kikipimwa na nikapata hati ya wizara, nitakuwa salama bila kuwa na hofu na wapora ardhi, lakini nimejua pia umuhimu wa kulipa kodi ya ardhi pamoja na jengo," alisifu.


SHREE SANATAN DHARMA SABHA

**NOTICE OF EXTRA ORDINARY GENERAL MEETING .**

The extra ordinary general meeting will be held on Sunday, 6th June 2021 at Shree Laxminarayan Mandir at 04:00pm- Pramukh Swami Grah. All members of Tanzania hindu community are required to attend on time.

The Agenda of the meeting are as follows:

**AGENDA**

1. Approval of audited accounts for 2020.
2. Reappointment of statutory auditors for 2021.
3. Approval of Budgets for 2021.
4. Approval of Shree Sai Temple plan.

The copies of accounts are available for viewing at the SSDS office (Monday to Thursday 5PM to 8PM) and please write your questions with details in the register at office before Friday 4th June, 2021, all queries will be addressed in the meeting.

The details of proposed Sai Mandir Plan will be circulated in the Social Media and will be available for review at SSDS office.

Thank you

**Yash Desai**
**Hon. General Secretary**
**Shree Sanatan Dharma Sabha**

*Providing Unity and Religious Leadership to the Hindu Community of Tanzania*

**Shree Sanatan Dharma Sabha**
Pramukh Swami Street
P. O. Box 5
Dar es Salaam, Tanzania

**Telephone:** +255 22 2132835
**Mobile:** +255

**Society Registration No:** 463
**TIN:** 101-321-207

**E-mail:** mandir@ssds.or.tz

**Web page:** www.ssds.or.tz

**A member of The Hindu Council of Tanzania**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kilio kodi taulo za kike kisikike

**KILA** mwaka kinapofika kipindi cha bajeti, kilio kikubwa kwa serikali ni kuangalia uwezekano wa kuondoa kodi kwenye bidhaa ya taulo za kike.

Wanaoteseka zaidi katika matumizi ya bidhaa hiyo ni wanafunzi ambao hutegemea msaada wa wazazi au walezi wanapofikia umri wa utu uzima wa kuitumia bidhaa hiyo.

Tumesikia wanafunzi wengi wa kike wakikosa vipindi vya masomo kwa muda fulani kila mwezi kwa sababu wanapofikia muda huo wanakuwa katika wakati mgumu kwa kukosa taulo za kuwasitiri hali inayowafanya wabaki nyumbani kwa kuona aibu ya kuchekwa na wenzao wa jinsi nyingine.

Hali hiyo pia huwasababishia kutofanya vizuri katika masomo yao.

Baadhi ya watoto hao, wazazi au walezi wanakosa uwezo wa kumnunulia mtoto kila mwezi kutokana na hali ya uchumi wa kipato.

Mtoto wa kike anapokuwa katika hali ya kutumia bidhaa hiyo, anatakiwa kuwa katika usafi wa hali ya juu ili asiweze kupata madhara kiafya. Kutumia mbadala wa bidhaa hiyo ni kuhatarisha afya ya mtoto wa kike na wengine kuwaathiri pia kwenye uzazi.

Kutokana na umuhimu wa bidhaa hiyo, juzi Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, akiongea katika maadhimisho ya siku ya hedhi duniani, aliomba Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), kukaa na wafanyabiashara wa taulo za kike kuangalia tena upya namna ya kupunguza kodi zinazotozwa kwenye bidhaa hiyo ili ipatikane kwa bei nafuu.

Ombi hilo la Naibu waziri limetokana na bidhaa hizo kupatikana kwa gharama ambazo hazilingani na kipato cha wanawake wengi wa kitanzania na wanashindwa kumudu kununua.

"Hali hii huwalazimu kutumia vifaa visivyo salama wakati wa hedhi na baadhi ya mabinti kutokwenda shuleni wakiwa kwenye hedhi," alisema.

Ikiangaliwa pia bidhaa hizo nyingi zinazalishwa nje ya nchi na kufanya gharama za kuagiza zikiunganishwa na kodi hufanya bei iwe juu zaidi.

TRA pia imetakiwa kuelimisha wafanyabishara ili kuzingatia bei elekezi kama ilivyo kwa bidhaa nyingine zinazopata bei elekezi serikalini.

Katika kuwaweka salama watoto wa kike hasa wanapokuwa shuleni ni muhimu ikatengwa bajeti kwa kwa ajili ya watoto hao ya kuwanunulia taulo za kike.


Naibu Meya wa Mansipaa ya Ubungo, Hassan Siraji, akitoa msisitizo katika maadhimisho ya siku ya hedhi duniani, kwenye eneo lake, anasema kama mtoto atashindwa kujistiri hawezi kushiriki masomo vizuri.

Kadhalika, amependekeza kila shule kuwe na vyumba maalumu vya kujistiri ili watoto waweze kujisikia huru wakati wote wanapokuwa katika hali hiyo shuleni.

Naibu Meya huyo aliwataka walimu kutoa elimu kwa watoto wa kike wajue hedhi ni kitu kilicholetwa na Mungu kwa ajili ya mwanamke.

Kwa kuzingatia uhimu wa bidhaa hiyo kwa watoto wa kike, kuna kila sababu kodi ikaangaliwa upya kama sio kuondolewa kabisa basi ipunguzwe ili kila mwanamke aweze kuipata.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

### Jamii ishiriki vita dhidi vifo vya wajawazito, watoto

**KATIKA** mwaka wa fedha wa 2021/2022, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inatarajia kutumia Sh. trioni 1.077, kwa ajili ya kuboresha huduma za afya nchini.

Miongoni mwa huduma hizo ni kuboresha utoaji wa chanjo ili kuwakinga watoto chini ya miaka mitano, wajawazito na kutoa chanjo nyingine za kimkakati za kukinga na kudhibiti magonjwa yanayozuilika kama homa ya ini.

Lakini pia wizara husika inasema, inatarajia kuendelea kupunguza vifo vya kinamama na watoto wachanga vinavyotokana na uzazi, kuimarisha huduma ya lishe na kuboresha usafi wa mazingira nchini.

Kimsingi, yapo mengi ambayo wizara inajipanga kiyafanya, lakini kikubwa zaidi, ninataka kujadili suala la afya ya uzazi ambayo ni mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa ili kuepusha vifo vinavyojitokeza kutokana na uzazi ili mjamzito na mtoto waweze kuwa salama.

Hapa si serikali pekee, bali ni vyema jamii nayo ikashiriki kuhimiza wajawazito kujifungulia hospitalini au kwenye vituo vya afya, ili kuwaepusha na vifo vinavyotokana na wao kuamua kujifungulia nyumbani.

> **Hapa si serikali pekee, bali ni vyema jamii nayo ikashiriki kuhimiza wajawazito kujifungulia hospitalini au kwenye vituo vya afya, ili kuwaepusha na vifo vinavyotokana na wao kuamua kujifungulia nyumbani.**

Jamii ikishiriki kuwaelimisha kinamama umuhimu wa kuhudhuria kliniki mapema wanapogundua tu kuwa wana ujauzito, hatua hiyo itasaidia kuwaepushia athari mbalimbali zinazoweza kujitokeza wakati wa kujifungua.

Hatua hizo na nyingine nyingi, zinaweza kusaidia pia kufikia malengo ya maendeleo endelevu ya millenia kuhusu afya ifikapo mwaka 2030 ambayo ni kuwa na raia wenye afya bora.

Kwa maana hiyo, ni wazi kwamba, kila mmoja wetu ana mchango wake katika kuhamasisha kinamama kuhudhuria kliniki kipindi chote cha ujauzito na cha kujifungua, ili waweze kujifungua salama.

Wataalam wa afya wamekuwa wakisema, wapo wajawazito wanaofariki dunia wakati wa kujifungua, hali inayochangia baadhi ya familia kupoteza kinamama kila mwaka.

Kuna kampeni kama 'Jiongenze Tuwavushe Salama', yenye lengo la kupunguza na kudhibiti vifo vitokanavyo na uzazi, lakini pia Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inatarajia kuibuka na nyingine.

Hiyo ni ya mfumo wa ufuatiliaji wa taarifa za wajawazito wote tangu wanapofika kliniki mara ya kwanza hadi baada ya siku 42 za kujifungua.

Waziri mwenye dhamana, Dk. Dorothy Gwajima, anasema, mfumo huo pia utasaidia wataalam wa afya kujua maendeleo wajawazito tangu wanapofika kituo cha afya siku ya kwanza hadi baada ya kujifungua.

Kwamba watapata taarifa zake kila siku ili kujua ni namna gani baada ya kujifungua wamehudumiwa ili wataalam hao wachukue hatua pale wanapoona kuna tatizo.

Dk. Gwajima anasema hayo kwa wataalam wa afya katika kikaokazi cha maandalizi ya utengenezaji wa mfumo huo na kuwataka wawe wanawafuatilia wajawazito inavyotakiwa ili kupata taarifa sahihi.

Kwa kampeni hizo na nyingine zinazoendelea kuibuliwa kwa lengo la kupunguza vifo vya wajawazito na watoto, ni wazi kwamba kuna uwezekano wa kupunguza tatizo iwapo kila upande utatimiza wajibu inavyotakiwa.

Cha muhimu kutambua ni kwamba, mtindo wa kujifungua nyumbani umeshapitwa na wakati, hivyo wale ambao hawajui hilo, si vibaya wakaelimishwa ili watambue umuhimu wa kuhudhuria kliniki.

Kadri miaka inavyokwenda, ndivyo magonjwa nayo yanazidi kuongezeka, na ndivyo umuhimu wa wajawazito kuhudhuria kliniki na pia kujifungulia hospitali kwenye vituo vya afya unaongezeka.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Hongera DPP ikikupendeza anza kusafisha uchafu uliokuta



Na Pascal Mayalla

**Kifungu cha 91 kimempa DPP mamlaka ya kuondoa mashtaka dhidi ya mtuhumiwa yeyote na kifungu cha 98, DPP anaweza kumfutia mashtaka mtuhumiwa yeyote kwa kutumia kitu kinachoitwa Nolle Prosequi, uamuzi wa DPP....**

KWA Maslahi ya Taifa ni safu ya mwandishi Pascal Mayalla, itakayochambua hoja mbalimbali za kisiasa, kiuchumi na kijamii kuhusu Taifa la Tanzania, kitaifa na kimataifa, kwa kutanguliza mbele maslahi mapana ya taifa.

Ni mwananchi, mwanahabari wa kujitegemea na mwanasheria, anaandika katika nafasi zote tatu; Kwanza kama Mtanzania wa kawaida, kwa kutumia haki na uhuru wa kutoa maoni; pili kama mwandishi wa habari mwenye wajibu wa kuhabarisha na kuelimisha jamii, tatu kama mwanasheria kusaidia kuwatetendea haki Watanzania, haswa pale ambapo haki zinaonekana kukiukwa wazi wazi, na huku Katiba, sheria, taratibu na kanuni zipo, lakini ama zinapuuzwa, ama zinakiukwa.

**KANUNI ZA MSINGI ZA HAKI ZA KISHERIA**

Tanzania inafuata Mfumo wa Sheria wa Kiingereza, ambao uliingizwa nchini toka tulipotawaliwa na Waingereza. Mfumo huu wa utoaji haki unafuata kanuni za msingi za haki za binadamu, ambazo ni pamoja na usawa mbele ya sheria, kila mtu atahesabiwa hana hatia, mpaka hatia ithibitishwe, jukumu la kuthibitisha hatia, ni mshitaki, hakuna mtu kuhukumiwa bila kusikilizwa, hakuna mtu anayeshtakiwa mara mbili kwa kosa lile lile na baada ya kuhukumiwa, mtuhumiwa ana haki ya kukata rufaa, na haki nyingine nyingi.

**DPP NA MAMLAKA**

Mfumo wa mashtaka nchini Tanzania, uko chini ya mtu anayeitwa Mkurugenzi wa Mashtaka, yaani DPP, ambaye anateuliwa na rais kwa mujibu wa ibara ya 59. Huyu DPP, ndiye mtu pekee mwenye mamlaka yote kuanzisha na kuendesha mashtaka yote ya jinai nchini Tanzania.

Mkurugenzi wa Mashtaka pia amepewa mamlaka chini ya kifungu cha 90 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, ana mamlaka ya kuanzisha mashtaka yote ya jinai dhidi ya mtu yeyote mbele ya mahakama zote isipokuwa ya mahakama ya (kijeshi na mahakama ya katiba). Kifungu cha 91 kimempa DPP mamlaka ya kuondoa mashtaka dhidi ya mtuhumiwa yeyote na kifungu cha 98, DPP anaweza kumfutia mashtaka mtuhumiwa yeyote kwa kutumia kitu kinachoitwa Nolle Prosequi, uamuzi wa DPP, hauingiliwi, wala kuhojiwa na mamlaka yoyote, hata rais wa JMT (Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

Kwa hivyo DPP, ni mtu mwenye mamlaka kubwa sana ya ajabu. Mtu mwingine mwenye mamlaka ya kufanya lolote bila kuwajibika kutoa sababu zozote kwa yeyote ni Rais wa JMT. Hivyo kwa mamlaka haya ya DPP, yakitumiwa vibaya, DPP ni kama mungu mtu, hivyo mtu mwenye mamlaka makubwa hivi anapokuwa hatendi haki, mfumo mzima wa utoaji haki unaathirika na kuonekana hautendi haki.

**HAKI INAPOCHELEWESHWA**

Kuna watuhumiwa ambao wanashtakiwa na Serikali ya Tanzania na kukaa muda mrefu mahabusu kwa sababu ya kukiukwa kwa kanuni za asili za msingi wa utoaji wa haki.

Hivyo, namuomba DPP mpya, kama itampendeza, jukumu lake la kwanza liwe kuangalia upungufu wote uliojitokeza ili kuepuka 'karma' ya vilio vya machozi, jasho na damu ya watuhumiwa kutotendewa haki.

DPP mpya, aanze kwa kutenda haki kwa kesi zote ambazo zimekuwa zikitajwa mahakamani kwa miaka mingi bila kusikilizwa kwa madai uchunguzi haujakamilika, huku watuhumiwa wakisota rumande na magerezani na wengine hadi wakipoteza maisha magerezani bila kutendewa haki.

Haki iliyocheleweshwa ni haki iliyo kiukwa, na haki, haipaswi tu kutendeka, bali haki inapaswa kutendeka huku ionekane kuwa imetendeka.

Hivyo namshauri DPP mpya arejeshe imani ya umma kwa ofisi ya DPP kwa kuwatendea haki Watanzania na watuhumiwa wote.

**Pascal Mayalla**
**Mob. +255 754 270403**
**pascomayalla@gmail.com**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Siasa za Bongo kama tamthilia



Na Joseph Kulangwa

**Asilimia iliyobaki 20 wakasema ni wakati mwafaka sasa, kuruhusu watu kujibweda na vyama vingi, ili CCM ipate kupingwa, kwa sababu imebweteka na kudhani bila yenyewe hakuliki wala hakulaliki.**

MIAKA ya mwanzo ya tisini, Mwalimu Julius Nyerere akiwa bado hai lakini mstaafu, Rais Ali Hassan Mwinyi aliunda tume ya kutafuta maoni ya wananchi kuhusu nchi kurejea kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Alhaji Mwinyi akamteua Jaji Francis Nyalali kuongoza tume iliyozunguka nchi nzima kusaka na kuratibu maoni ya Watanzania wa wakati huo, waliokwishazoea kuwa chini ya chama kimoja, Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Watu waliokuwa wakiishi maisha ya amani na utulivu, lakini yenye ukata ulioambukizwa na vita vya Kagera, wakasema acheni tufe na CCM yetu tu, hata kama mlo ni mmoja.

Asilimia 80 ya waliohojiwa wakasema hatutoki hapa.

Asilimia iliyobaki 20 wakasema ni wakati mwafaka sasa, kuruhusu watu kujibweda na vyama vingi, ili CCM ipate kupingwa, kwa sababu imebweteka na kudhani bila yenyewe hakuliki wala hakulaliki. Piga ua hakuna kuikumbatia CCM.

Hatimaye taarifa ikawasilishwa kwa Rais Mwinyi, kwamba Watanzania ni wagumu, hawataki katu mabadiliko, hata iwe nini wako tayari kubaki na CCM, liwake jua inye mvua, hakuna kubadilisha mfumo wa utawala ni chama kimoja tu basi.

Vichwa vikawauma wanatume ya Nyalali, hakika hata Mwalimu Nyerere kichwa kikamuuma, akiona jinsi dunia inavyobadilika kwa mwendokasi, akasema hapana lazima tubadilike tu. Wakamfuata kwa ushauri akasema: "Wengi wape lakini wachache nao wasikilizwe."

Sasa ili kauli hii ipate mashiko, ilikuwa lazima kuwe na sababu za ziada za kutengua usemi huo ambao ni wa wahenga, na umedumu maisha yote duniani hakuna aliyepata kuutengua.

Siku zote lilipoamuliwa jambo kwa kura, jibu lilikuwa ni wengi wape, baasi.

Leo anakuja mtu anasema, sawa wengi wape ndiyo, lakini wachache nao wasikilizwe. Kwa kuwa aliyesema hayo alikuwa ni Mwalimu na kwa kuwa alikuwa mahiri katika kuelimisha, akawaambia jamani dunia inatuacha, tukibaki hapa tutaishia.

Kwa heshima ya Watanzania kwa baba yao wa Taifa, wakaona isiwe tatizo, wakakubali. Mwaka 1992, Tanzania ikarejea rasmi kwenye nfumo wa vyama vingi. Nchi ikawa sasa na upinzani rasmi. Wakaibuka kina Edwin Mtei kuanzisha Chama cha Demokrasia na Maendeleo.

Wakaibuka kina James Mapalala na KAMAHURU kasha CUF, tukawasikia kina Mabere Marando na kina Bob Makani, kina Walid Kabourou wakitoka Marekani kuja kufanya mambo, wakishirikiana na kina Freeman Mbowe wakiwa vijana barubaru.

Tukaanza kuwasikia kina Christopher Mtikila, kina Prince Bagenda, kina Chifu Abdallah Fundikira, kina Ndimara Tegambwage, Kamara Kusupa na wengineo wengi, wengine wakahama CCM na kujiunga na upinzani watu kama Augustine Mrema na wengi, wengi wengine.

Nchi ikawa kama ikapamba moto, nchi ikachemka, ikademka nakwambia, maandamano huku na kule, mikutano ya hadhara na kila aina ya hekaheka. Tukawasikia kina Profesa Baregu nao wakishuka kutoka Mlimani kuja kushajiisha mapambano ya kisiasa.

Watu ikawa niende huku mara niende kule, mambo haihai, kaulimbiu kedekede, 'Saa ya Ukombozi ni Sasa', mara 'Haki kwa kila mtu'. Tukasikia misamiati ya Magabacholi, ikihanikizwa na Mtikila na chama chake cha DP.

Baadaye wakaibuka kina James Mbatia, kina Zitto Kabwe na hivi karibuni kina Tundu Lissu, wakisimama dede kukabiliana na jimwamba CCM, ambalo limeota mvi katika mapambano ya kisiasa likishika Dola linavyotaka. Wakiingia kulisukumiza pembeni lakini wapi, kila mara wakirudi kujipanga upya.

Hata hivyo, kila wakijipanga ndivyo walimomonyoka. Wakaribisha watu kama kina Edward Lowassa, Frederick Sumaye, Nyalandu na wengine, unakuwa moto wa kifuu tu, baadaye hao wanarudi nyumbani kusimulia walichokiona upande wa pili.

Hivi sasa upinzani nchini ni kama mchezo wa kuigiza tu, wapinzani wakichukuliwa kama kama wanasesere wa watoto kulingishiana. Ona sasa lile kundi letu pendwa la Covid-19 liko bungeni, lakini haijulikani nani kalipeleka huko, si chama si Katiba ya nchi, wapo tu, wakila na kusaza! Siasa za Bongo ngumu!

**Alamsiki!**

SAFU

## KONA YA UKWELI

# Kipi kinashindikana kumkamata mtuhumiwa huyu?



Na Thobias Mwanakatwe

TAREHE 16 Mei 2021, Mkurugenzi wa Kituo Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, pamoja na baadhi ya wanasheria walifanya ziara katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya kufuatilia sakata la wanafunzi wawili wa Shule ya Sekondari Itope wanaodaiwa kutoroshwa na mfanyabiashara mmoja wa mjini Kyela.

Wanafunzi hao (majina tunayahifadhi) wa kidato cha pili katika shule hiyo wanadaiwa kutoroshwa na mfanyabiashara huyo tangu mwezi Januari, mwaka huu na mpaka sasa hawajulikani waliko hali inayoleta simanzi na vilio kila siku kwa wazazi.

Baada ya kutoroshwa, taarifa ziliripotiwa katika kituo cha Polisi Kyela mjini na kupewa RB namba KY41/RB/07/2021 na ISK/RB/41/2021, lakini tangu taarifa za tukio hilo zitolewe mtuhumiwa hajakamatwa ikiwa ni takribani miezi mitano sasa.

Wazazi wa wanafunzi hao kwa muda mrefu wamekuwa wakifuatilia polisi kujua hatima ya watoto wao na kama mtuhumiwa amekamatwa, lakini kimekuwa ni kitendawili kisichokuwa na majibu ambapo haijulikani kama wapo hai au wameshakufa.

Kutokamatwa kwa mfanyabiashara huyo ambaye hadi sasa biashara zake za maduka zinaendelea kama kawaida mjini Kyela sambamba na ujenzi wa nyumba zake mpya ndiko kulikomsukuma Mkurugenzi wa LHRC kuchoma mafuta ya gari na kutembea umbali wa zaidi ya kilometa 900 hadi wilayani Kyela.

Mkurugenzi wa LHRC awali aliwatuma maofisa wake, lakini hakukuwa na matokeo chanya na safari hii akaamua kwenda mwenyewe kujionea kulikoni mfanyabiashara huyo hakamatwi huku taarifa za kiintelijensia zikionyesha mtuhumiwa yupo hapa hapa nchini.

Kituo cha kwanza baada ya kuwasili Kyela, Mkurugenzi wa LHRC alionana na mzee Simon Mwasitu nyumbani kwake karibu na njiapanda ya kwenda mpaka wa Kasumulu ambaye mtoto wake anadaiwa kutoroshwa kwa mara pili na mfanyabiashara huyo.

Mzee Mwasitu anaanza kwa kueleza kuwa sakata la kutoroshwa mwanaye ameshakata tamaa kabisa kuendelea kulifuatilia polisi kwa madai kuwa Jeshi la Polisi limeshindwa kumtia mbaroni mfanyabiashara huyo kwa muda mrefu sasa bila sababu za msingi.

Anasema suala hilo ameamua kulikabidhi mikononi mwa Mungu kwani hivi sasa limeanza kumletea matatizo kifamilia na pia kuishi maisha ya wasiwasi ambapo wakati mwingine anafungiwa kwa nje mlango wa nyumba yake na watu wasiojulikana bila kufahamu lengo la watu wanaofanya kitendo hicho.

Anaongeza kuwa anaimani kubwa na LHRC kwamba wataweza kufuatilia kwa kina tukio hilo na haki itaweza kutendeka na kwamba anachomuomba Mungu kila siku ni mtoto wake apatikane akiwa salama.

Baada ya mazungumzo na mzazi huyo, msafara wa Mkurugenzi wa LHRC na timu yake ukatinga katika Shule ya Sekondari Itope iliyopo nje kidogo na Kyela mjini ambako wanafunzi hao walitoroshwa.

Mkuu wa Shule na mwalimu wa nidhamu na malezi wa shule hiyo wanamthibitishia Mkurugenzi wa LHRC kutoroshwa kwa wanafunzi hao na kwamba na wao wanasikitishwa sana kwani 'wanamiss' masomo hasa ikizingatia kuwa kuna mtihani wa taifa wa kidato cha pili mbele yao ambao unatarajia kufanyika mwezi Novemba, mwaka huu.

Baadaye ikafuata zamu ya kwenda kituo cha polisi Kyela mjini ambapo hapa Mkurugenzi wa LHRC na timu yake wakapata wasaa wa kuonana na Mkuu wa Kituo ambaye naye kwasababu ya ugeni akasema jambo hilo halifahamu vizuri na kumwita mpelelezi wa kesi hiyo.

Mkurugenzi wa LHRC swali lake la kwanza kwa mpelelezi wa tukio hilo lilikuwa ni kutaka kujua kwanini jeshi la polisi limechukua muda mrefu kumkamata mtuhumiwa aliyetorosha wanafunzi hali ambayo imezua hofu na maswali mengi yasiyo na majibu juu ya nguvu alizonazo mfanyabiashara huyo hadi asikamatwe.

Ziara ya Mkurugenzi wa LHRC ilihitimishwa kwa kuonana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, ambaye baada ya mazungumzo ya kina aliahidi kutoa ushirikiano ili mtuhumiwa huyo aweze kukamatwa ndani ya mwezi mmoja na kuchukuliwa hatua kwamujibu wa sheria.

Kimsingi ukiyasikiliza maelezo ya mzazi, walimu na jeshi la polisi katika sakata hili utabaini kuna jambo nyuma ya pazia na ndio maana intelejensia ya polisi Mbeya ni kama imekwama au imeshindwa kumtia mbaroni mtuhumiwa.

Haiingii akilini mtuhumiwa atafutwe kwa miezi mitano hapatikani, lakini wakati huo huo biashara zake ambayo ni maduka yanaendelea kufanyakazi kama kawaida na pia ujenzi wa nyumba zake mpya unaendelea na cha kujiuliza ni nani anatoa fedha za kuendeleza miradi yake hiyo.

Noja tusubiri mwisho wa muziki huu na mwezi alioahidi RPC ili tuone utachezwa kwa staili ipi.

**NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA….Kazi Iendelee**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA

# Fahamu umuhimu wa kumsikiliza mwenzi wako



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

**Lengo la makala hizi katika darasa hili la ndoa ni kuwasaidia wanandoa kuishi maisha bora ya ndoa. Unapojifunza usijitazame wewe tu, bali angalia familia yako pia.Kama una mtoto wa kiume ujue una mume wa mtu mtarajiwa.**

NDOA ni zawadi ya Mungu kwa mwanadamu. Ndoa sio taasisi ya kuivamia bali maandalizi yanahitajika. Bahati mbaya sana, watu wengi huelekeza nguvu nyingi zaidi katika kuandaa sherehe kubwa za harusi, kuliko kujiandaa kuwa mume au mke bora. Matokeo yake, watu wengi wameingia katika ndoa wakiwa hawana ufahamu na maarifa ya kutosha kuhusu taasisiya ndoa. Hali hii imesababisha migogoro na kuvunjika kwa ndoa nyingi. Upo umuhimu mkubwa kwa wanandoa na wanandoa watarajiwa kufahamu mahitaji na madai ya taasisi ya ndoa kabla na baada ya kuingia katika ndoa.

Maisha ni safari ndefu inayohitaji kujifunza na kukua kila siku. Kupata ufahamu mzuri kuhusu uhusiano wa ndoa ni zoezi la maisha yote ya wanandoa. Mtu anapooa na kuolewa afahamu kuwa anaingia katika shule ambayo haina kuhitimu.Hii ni hatua nyingine muhimu ya maisha ambapo uvumilivu unahitajika sana. Mungu alianzisha taasisi hii ili watu waingie, waipende na kuifurahia.

Hata hivyo, mambo yamekuwa kinyume kwa baadhi ya wanandoa. Wanandoa wengi wameshindwa kuishi maisha ya ndoa. Maisha ya ndoa ya baadhi ya wanandoa ni kama jangwa, ambapo muda wote hufukuta joto na kutimua vumbi. Wengi wao wamekuwa wanaharakati zaidi kuliko kuwa walezi wa ndoa zao. Usanii (Pretendence) unazidi kuongezeka katika ndoa nyingi.

Wakiwa mbele ya watu wengine hujifanya wako sawa na wanapendana, lakini maisha yao ya ndoa yamejaa migogoro na kutokuelewana. Hali hii imesababisha wanandoa wengi kupoteza hisia chanya na mvuto dhidi yao.

Lengo la makala hizi katika darasa hili la ndoa ni kuwasaidia wanandoa kuishi maisha bora ya ndoa. Unapojifunza usijitazame wewe tu, bali angalia familia yako pia.Kama una mtoto wa kiume ujue una mume wa mtu mtarajiwa. Kama una binti, basi ujue una mke wa mtu mtarajiwa.

Mafunzo haya yatakusaidia kuweka misingi bora ya maisha ya baadaye ya watoto wako pia, kwani watoto hujifunza sana kutokana na matendo ya wazazi wao. Pia, mafunzo haya yamekusudia kuwapatia ufahamu na maarifa vijana wanaotarajia kuingia katika ndoa ili wawe waume na wake bora.

Ni muhimu kuruhusu fahamu zetu kuingiza jambo jipya kwa kuwa kila siku ni siku ya kujifunza. Kujifunza huondoa kasumba ya kuishi kwa mazoea, hivyo, watu wapende kujifunza na kuruhusu mabadiliko ndani yao. Katika makala ya leo, tunajifunza umuhimu wa kumsikiliza mwenzi wako. Kupata muda wa kumsikiliza mtu mwingine ni zawadi ya thamani. Watu wengi wanajua kuongea, lakini watu wachache wanajua namna ya kusikiliza watu wengine.

Mara nyingi watu wana shughuli nyingi kiasi cha kushindwa kusikiliza watu wengine. Kumsikiliza mwenzi wako ni muhimu kwani zipo faida nyingi.

Faida na umuhimu wa kumsikiliza mwenzi wako

●Kusikilizwa ni sehemu ya tiba kwani mtu anapata fursa ya kueleza ya moyoni mwake.

●Unapomsikiliza mwenzi wako unampa ujumbe kuwa unajali.

●Kusikiliza kunakusaidia kuwa karibu na mwenzi wako kimwili na kihisia.

●Unapomsikiliza mwenzi wako unajifunza zaidi kutoka kwake.

●Kusikiliza kunawasaidia wanandoa kufahamiana zaidi. Mwenzi atafahamu kile mwenzake anachofikiri, mahitaji yake, hisia zake na matamanio yake.

●Kusikiliza ni ishara ya kumheshimu mwenzi wako.

●Unapokuwa msikilizaji mzuri wa mwenzi wako, unatoa ujumbe wenye kuonesha kuwa yeye ni mtu muhimu.

●Kumsikiliza mwenzi wako huongeza pendo, mahaba na mvuto.

Kwa hiyo, usimpuuzie mwenzi wako, bali tamani kumsikiliza. Jihadhari na mambo au vitu vinavyoweza kukufanya ukose muda wa kumsikiliza mwenzi wako, kwani baadhi ya wanandoa simu za kiganjani au kazi zimechukua muda wa wenzi wao na watoto. Ni muhimu kukumbuka kuwa, upo kwa sababu watu wengine wapo! Dhamiria kupata muda wa kumsikiliza mwenzi wako, halikadhalika na watoto wako pia.

Usipende wewe usikilizwe tu, lakini tamani kusikiliza mtu mwingine pia. Unaposikiliza unajitengenezea mazingira ya wewe kusikilizwa pia. Kusikiliza ni jukumu la msingi la upendo katika ndoa. Zingatia hii itakusaidia katika maisha ya ndoa na kuongeza thamani yako kwa mwenzi wako!

**[Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066].**

MAISHA

MEI 30, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili



Ukurasa 10

## Mzazi ni daraja la mtoto kutimiza ndoto yake



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Namna ya kufanya meza yako ya chakula kupendeza



## HARUSI

Ukurasa 12



'HEELS'

# Raha, karaha za viatu virefu

Ukurasa 14

# Mzazi ni daraja la mtoto kutimiza ndoto yake

**Na Beatrice Moses**



NENO la Mungu ndiye mpaji lina maana kubwa kwa yule ambaye anajituma katika kutafakari vyema mambo. Kila mtu ana kipaji chake ambacho Mungu amemkirimu.

Kazi ya mzazi kwa mtoto ni kumlea katika misingi ipasayo. Ikiwamo kuhakikisha anapata chakula, malazi na mavazi.

Pia ni wajibu wa mzazi kuhakikisha anasimamia na kugharamia elimu ya mwanaye. Hivyo kila mzazi anapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kuwa na kipato cha kulea watoto wake vizuri.

Ni wazi kwamba kuna ndoto njema ambazo mtoto huzipata kulingana na kipaji ambacho Mungu amemjalia, miongoni mwa vipaji hivyo ni pamoja na uwezo wa kuunda ama kubuni kitu vya aina mbalimbali, kucheza michezo, kuimba na vingineyo vingi ambavyo jamii inanufaika navyo.

Baadhi ya vijana waliofanikiwa kutimiza ndoto zao wamevuna yaliyo mema wao binafsi lakini pia wamewezesha kunufaisha ama kuburdisha jamii kwa kutumia vipaji vyao.

Kuna wakati inaweza kutokea mtoto akabadilishiwa kipaji chake kutokanana mazingira anayoishi, wapo ambao wamebadilishiwa na wazazi wao na wengine wamevumbua 'vipaji' visivyokubalika wala kuheshimika kwenye jamii, miongoni vipaji vinavyosababisha kero ni wizi.

Hivyo ni jukumu la mzazi kuhakikisha anakuwa kiongozi mzuri kwa mwanaye ili anafanikiwe kutimiza ndoto njema ya kipaji alichonacho, lakini jambo la kushangaza miongoni mwa wazazi ndiyo wamekuwa wakichangia kuharibu ama kubadili ndoto za watoto.

Wapo wawazi ambao nao wamekuwa wakiota ndoto za kuwa na watoto wenye vipaji vile wamavyovipenda wao, katika mazingira hayo wapo ambao wamelazimisha watoto kusomea masomo ya fani ambazo haziendani na vipaji ama ndoto walizonazo watoto hao.

Jambo hilo limesababisha baadhi ya watoto hao hata wanapofanikiwa kumaliza masomo hayo wanaokosa ushawishi wa kufanya kazi zinazoendana na fani walizosomea, hivyo inakuwa ni hasara kwa pande zote mbili mzazi na kijana wake.

Mfano kuna wazazi ambao hawatambui kuwa wanapaswa kuwasaidia vijana wao wenye vipaji kwa michezo mbalimbali ambayo ni fani na ina mafunzo husika hivyo wapelekwe kunakostahili ili waweze kuatimiza ndoto walizonazo.

Wapo pia wanaolazimisha watoto wawe wanamichezo hata kama mtoto hana kipaji huko, wazazi wa aona hii ndiyo wamekuwa wakichangia baadhi ya maeneo kukosa watu wenye sifa kwa kuwa walilazimishwa hivyo hawafanyi kwa moyo wa kupenda.

Mzazi ana mtoto ambaye anatamani kuwa mtaalam wa magari yeye anamlazimisha asomee udaktari au uhasibu hiyo siyo sawa, ni vyema kumtambua mwanao ana ndoto gani nawe ukasaidia umpitisha katika maeneo ambayo atafanikisha ndoto yake hiyo kutimia kadri Mungu atakavyomjalia.

Ni vyema kila mzazi akakumbuka wajibu wake wa kumjengea mtoto wake uwezo wa kutimiza ndoto anayoitamani ili iweze kumpa thamani katika maisha yake, hivyo anza kumuuliza mwanao mwenye uelewa je, anatamani kuwa nani baada ya kukua nawe usaidie kumpa mwongozo mzuri wa kufanikisha.

Jamii inatamani kuwa na vijana wenye vipaji vya aina mbalimbai, wenye ndoto njema ikiwamo za ubunifu wa vifaa mbalimbali vikiwamo hadi vile vya vinavyokwenda na sayansi na teknolojia.

## NA HAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

Andika kitenzi **Ouvrir** (yaanikufungua) katika nyakati tofauti kama zilivyoainishwa hapo chini.

**Indicatif**
**présent**
j' ..............
tu ..............
il/elle .............
nous...............
vous ...............
ils/elles ..............

**imparfait**
j' .......................
tu ......................
il/elle ....................
nous ....................
vous ...................
ils/elles .................

**future simple**
j' ...................
tu ...................
il/elle .................
nous ................
vous ................
ils/elles .......................

**passé simple**
j' .........................
tu ........................
il/elle ......................
nous ......................
vous .....................
ils/elles .....................

**passé compose**
j' ai ..............................
tu as .............................
il/elle a ............................
nousavons ............................
vousavez .............................
ils/ellesont ..............................

**plus – que – parfait**
j' ..........ouvert
tu .........ouvert
il/elle .........ouvert
nous..........ouvert
vous.........ouvert
ils/elles...........ouvert

**futurantérieur**
j' ...........ouvert
tu ...........ouvert
il/elle ..........ouvert
nous .............ouvert
vous ...........ouvert
ils/elles ..............ouvert


**passéantérieur**
j' eus ..............
tueus .............
il/elleeut .............
nouseûmes .............
vouseûtes ..............
ils/elleseurent ...............

**Conditionnel**
**présent**
j' ................
tu ................
il/elle ...............
nous ..............
vous ..............
ils/elles ................

**passé**
j' aurais ...................
tuaurais ..................
il/elleaurait ..................
nousaurions ..................
vousauriez ..................
ils/ellesauraient ..................

## WATOTO

## PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya Adaktari

SHUHUDIA jinsi mgambo walipokwenda kumkamata jamaa mmoja

**Mgambo:** Hodi, hodi
**Jamaa:** Kimya
**Mgambo:** Hodi, hodi wenye nyumbaa
**Jamaa:** We nani kwani?
**Mgambo:** Sisi mgambo
**Jamaa:** Sawa, mnataka nini?
**Mgambo:** Kuongea na wewe
**Jamaa:** Kuongea na mimi?!
**Mgambo:** Ndio
**Jamaa:** Mko wangapi?
**Mgambo:** Watatu
**Jamaa:** Kama mko watatu si muongee wenyewe...!!!

**SWALI**
Paka ana manufaa gani kwa binadamu?
5

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Kazini huambiwa ana harufu mbaya, nyumbani yupo vizuri, tatizo ni nini?

***KARIBU tena msomaji tuendelee kujadili yale yanayojiri kwenye maisha yetu kila uchao. Ni kama vile yanaonekana kuwa ni ya kawaida kumbe ni matatizo makubwa yaliyojificha na kufunika fahamu zetu.***

Nimegundua kwamba vijana wengi wameshikwa na maadui siyo tu kwenye eneo la mahusiano, bali uchumi. Shetani anajua fika kwamba akikamata maeneo hayo familia nyingi hazitakuwa na mafanikio katika maendeleo yao. Lazima vinakuwepo vikwazo ili mtu anayejitahidi kuinuka arudi chini.

Wiki iliyopita nilikuwa Morogoro kwa mkutano wa kikazi. Asubuhi wakati natoka hotelini kwenda kwenye mkutano, mama mmoja mfanyakazi wa pale akawa anaongea kwa simu kuhusu kijana wake aliyemnunulia pikipiki hivi karibuni ili ainasue familia kiuchumi.

Baadhi ya maneno niliyoyanasa ni kwamba kijana wake amekuwa na mvuto wa abiria kwenye kituo chao cha bodaboda. Kila anaporejea anapata abiria hadi wenzake wanashangaa.

“ Cha ajabu, Dula haendi tena kazini, pikipiki kaegesha nyumbani, nikimuuliza kwa nini anadai wateja pamoja na wenzake wanamwambia ananuka. Lakini anapokuwa nyumbani yupo sawa, hatusikii harufu yoyote mbaya, anasema na kuongeza;

“Hivi sasa yupo nyumbani anajifungia ndani analia tu, hata mimi nachanganyikiwa sijui nifanyeje”. Mama huyo alipomaliza kuongea kwa simu, nilimfuata kutaka nipate taarifa zaidi. Akasema ni miezi mitatu sasa akifanya kazi hiyo bila tatizo lolote.

Msomaji wangu, picha niliyoiona kwenye familia hii ni kwamba ipo vita imeanzishwa dhidi yake. Katika maisha, Mungu amewafungulia wanadamu milango ya mafanikio, tena mikubwa sana. Lakini wapo baadhi ya watu hupinga wenzao kupenya.

Shetani ana tabia ya kusubiri mtu aanzishe mradi, kisha yeye anavuruga. Kile ambacho unakitamani sana kukifanya, shetani naye amenyoosha mkono wake pale. Unanunua simu yako nzuri, adui anainyemelea anakuibia. Unabahatika kuwa na maisha mazuri, mke au mume mzuri lakini wapo watu wabaya wanawakodolea macho wakitamani kuibomoa ndoa yako. Chochote kile unachokipenda, amini kuwa mkono wa giza nao umekishikilia.

Ukitaka kuinuka juu lazima uchukue hatua. Na zaidi ya yote, kile unachotaka kukifanya ni lazima ujiandae kwa vita. Kama huna nguvu ya Mungu ya kukusaidia, utapata taabu sana. Katika vita hiyo ni lazima uwe na nguvu zaidi ya adui yako ndipo utaweza kumshinda. Hiyo ni kanuni katika ulimwengu wa roho.

Familia ya kijana niliyemtolea mfano, iliamini kuwa maadam imejipatia chombo cha usafiri, bodaboda, huo ni mwanzo wa kujikwamua kiuchumi. Kumbe, badala yake ndio kwanza wameingia vitani.

Msomaji wangu, kumbuka wapo baadhi ya watu wanatumia sana nguvu za giza kuinukia kiuchumi. Hawa wanainuka haraka lakini mara nyingi anguko lao ni kubwa sana. Katika biashara michezo ya kishirikina ni mingi wengine hufikia hatua kupotezeana maisha.

Lakini pia lipo kundi linalomtegemea Mungu. Wanaanza taratibu, baadaye kipato kikaongezeka na kudumu. Nguvu ya Mungu huwaweka salama hata adui akiwapiga hawayumbi.

Vijana wengi wanaofanya biashara ya bodaboda wamekuwa kama wamepagawa hawatulii wakifukuzia abiria. Kijana mmoja mlokole nikataka kujua afanyavyo kazi na majaribu anayokutana nayo.

Akasema; “Hapa unavyotuona kituoni wapo wanaokwenda nyumba za ibada, wengine wanategemea nguvu za giza kuvutia abiria. Hupeleka vyombo kwa waganga na kupewa hirizi za kinga.

Kundi lingine hawaendi nyumba za ibada, wanachojua ni kupata fedha akishatoa za tajiri zingine ni ulevi na starehe. Baadhi hujitambua na kujenga nyumba hata kuoa.

Kwa wale wanaoendekeza nguvu za giza wamekuwa na wivu kwa wenzao wanaoinuka kimaendeleo. Ni vita ya kuangushana badala ya kutiana moyo. Ndivyo anavyomaliza kusema kijana huyu.

Mpenzi msomaji, baada ya maelezo hayo, nikarudisha picha kwa kijana wa Morogoro. Nikawaza pengine huyu hakuwa na nguvu ya Mungu kumkinga na mashambulizi ndio maana akarushiwa mkosi wa harufu abiria wamkimbie. Hii ndio vita inayowakuta baadhi ya vijana wetu. Wengine hatma zao zimepindishwa, wengine ndoto za mafanikio zimekatishwa ghafla kwa ajali visababishi ikiwa ni ulevi na ushirikina.

***Msomaji wangu, Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki ijayo nitaelezea zaidi jinsi watu wanavyoishi na vifungo vya maisha wasijue cha kufanya. Je, una maoni, kisa, tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Siasa iwekwe kando suala la machinga, mama lishe

WIKI iliyopita Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alitoa maelekezo ya kuwa na utaratibu wa wafanyabiashara ndogo maarufu kama machinga, na mama lishe ili kuhakikisha jiji limepangika.

Agizo hili limekuja kwa wakati mwafaka kwa kuwa jiji la Dar es Salaam, sasa linaonekana chafu na halina mpangilio kwamba mtu yeyote anaweza kufanya biashara kokote bila kuulizwa na yeyote na kutolipa kodi yoyote.

Kwa sasa njia za watembea kwa miguu hazipo ndiko wafanyabiashara hao wamejaa na mbaya zaidi walirudi hata katika maeneo wasiyotakiwa kama Posta, na kubwa ni siasa kupewa nafasi kubwa kuliko uhalisia, kwamba hawa ni wapiga kura wasibughudhiwe.

Ukienda Kariakoo idadi ya machinga imeongezeka kiasi kwamba hakuna pa kupita, na wamepanga bidhaa zao nje ya maduka, wateja wengi wadogo wanaishia kununua kwao huku wenye maduka ndiyo wanaolipa kodi.

Ukienda Mwenge idadi inaongezeka kiasi kwamba kwa sasa hakuna sehemu za maegesho ya magari, huku maeneo ya watembea kwa miguu yaliyojengwa hivi karibuni kutokana na upanuzi wa barabara ya Mwenge Morocco wameshajaa.

Ukienda Mbagala ndiyo kabisa wamejipanga hadi eneo la katika la hifadhi ya barabara na huku maeneo ya watembea kwa miguu yakimezwa yote.

Hali hii siyo ya kuridhisha kabisa kwani jiji linakuwa na miavuli au mifuko ya nailoni mingi iliyosambazwa ili kupata kivuli huku usiku wakisambaza umeme ili kupata mwanga, jambo ambalo ni hatari.

Wafanyabiashara wenye maduka wanalipa kodi, lakini wanashindwa kufanya biashara kiasi kwamba baadhi wamefunga maduka na kugeuza kuwa stoo za kuhifadhi mizigo, ambayo husambazwa kwa wafanyabiashara ndogo na sasa ile kodi ambayo serikali ilikuwa inapata haipati tena.

Ni muhimu sana kukawa na utaratibu kwa kuwapanga wafanyabiashara hawa kwa kuwa siyo kweli kuwa wanaruhusiwa kufanyabiashara zao kila mahali, ni lazima kuwe na nidhamu ya ufanyaji biashara, na siyo kwamba wakifanya hivyo ndiyo wapiga kura wazuri. Haya yalifanyika kwenye mapito ya wanyama na maeneo ya mtawanyiko, ambayo yanapotea kwa kuwa vimesajiliwa vijiji, kufunguliwa mashamba na ofisi za serikali, kwa kisingizio cha wapiga kura.

Hali hii iko katika miji yote, na wakati utaratibu unafanyika ni muhimu kufungananisha sekta kama miundombinu mizuri na nishati, ili kuongeza mzunguko wa biashara kwenye miji midogo kwa ajili ya kupunguza wimbi la vijana wanaokimbilia mjini.

Mathalani, ukitembelea soko la Mabibo, Buguruni, Kariakoo na kwingine kuna idadi kubwa ya wavulana wanauza mifuko na kubeba mizigo, baada ya muda hao ndiyo hugeuka kuwa machinga na kuanza kupanga bidhaa kando ya barabara.

Kwa ujumla serikali inapoteza mapato mengi kwa kuruhusu watu hawa kuongezeka, na wapo ambao hawakubali kuonyesha wamekuwa kibiashara kwa kuwa wanajua kinachofuata ni kulipa kodi.

Agizo la kuwapanga ni muhimu sana likatekelezwa hata kwa kujifunza nchi nyingine ambazo zimefanikwa, kwamba waliweka kando siasa ya kwamba hawa wasibugudhiwe ni wapiga kura.

Ukitembelea Jiji la Bangkok, Thailand, wametenga maeneo ya mama lishe ambao wapo kwenye jengo kubwa katikakati ya mji, huku kwenye mitaa kuna eneo maalum na siyo kila mtu kujipangia bidhaa au kuanza kuuza chakula pale anakoona yeye kunafaa.

Pia, kwa machinga wamepanga vizuri sana kiasi kwamba unaingia kwenye jengo kubwa lina machinga wa kila aina, na ndicho kinatakiwa kufanyika kwamba Kariakoo kuwe na maduka ya wauzaji wakubwa na machinga ambao wako kwenye eneo moja.

Hali ya sasa inaumiza nchi kwamba wale wanatakiwa kufanyabiashara ili walipe kodi wanashindwa na sasa kuna ujanja wa kufunga maduka na kubaki na stoo ya kuhifadhi mizigo inayosambazwa kwa machinga, hali ikiachwa hivi siyo sawa.

Jiji la Dar es Salaam linapaswa kupangwa na ndiyo itakuwa mfano kwa miji na majiji mengine, kuacha hali ilivyo ni kuharibu muonekano ambao siyo lazima mgeni atembelee bali akiwa angani anaona jinsi tulivyokosa mpangilio.

Machinga ni Watanzania na wanahaki ya kutafuta kipato, lakini lazima kuangalia kasi ya vijana na kukimbilia mjini, na kuhakikisha kuna kuwa na ukuaji sawa wa miji na majiji, na kujenga mazingira wezeshi kwa vijana kubaki vijijini kuzalisha na kupata mkate wa siku.

Wengi wanakimbilia mjini kwa kuwa ndiko kuna uwezekano wa kupata kipato, na bado shughuli za kilimo, uvuvi na ufugaji hazijajengewa mazingira wezeshi ya kuendelea kusalia waliko.

***Mungu ibariki Tanzania***

# HARUSI





SHANGWE na nderemo zilisikika kwa wanafamilia ya bwana harusi Mburuja Mmbata na Bi Irene Mngazija ambao waliamua kufunga ndoa Aprili 18, mwaka huu na kufuatia sherehe ya kuwapongeza iliyofanyika Mkonge Hoteli jijini Tanga.





MITINDO







KAUNDA SUTI

# Vaa upendeze msimu wote

MSIMU wa baridi unaendelea, kila mtu anakuwa makini kujilinda kwa kuvaa nguo ambazo anagalu zinaongeza joto na kumpa mwonekano wa kupendeza.

Mavazi aina ya Kaunda suti zilizobuniwa kisasa ni baadhi ya mavazi ambayo kipindi hiki yanabamba vilivyo.

Kulingana na mbunifu wa mavazi Katonda, nguo za Kaunda suti zinavaliwa na watu wa aina zote, wanawake na wanaume kutokana na sifa yake kubwa kuwa inafaa kwenda nayo sehemu yoyote. Aina hizi za nguo zinatumia vitambaa aina ya tiara, ambavyo ni vizito na vyenye rangi inayong'aa na kumpatia mtu husika taswira nzuri mbele ya jamii.

Endapo utanunua Kaunda suti, una uhuru wa kuvaa viatu vya aina yoyote ili mradi inalingana na rangi ya nguo yako tu. Unaweza kuvaa viatu vya ngozi, sendo au 'simple'. Ukitaka kuvaa kofia kichwani, basi chukua ya umbo la duara, halafu weka nakshi murua ya mawani na saa kwenye mkono wako wa kushoto.

Wengi wanaona vazi hili lina gharama kubwa, lakini kiuhalisia ni ndogo ukilinganisha na suti zingine zinazopatika madukani. Nipo lebo ya 'Katonda Dis' Gongolamboto kwa Diwani. Mavazi ya 'Kaunda suti' za Kisasa.

***(Kwa msaada wa Katondo Design, anayepatikana Gongolamboto jijini Dar es Salaam. Simu 0622246311, 0769316940)***





UREMBO



## ‘HEELS’

# Raha, karaha za viatu virefu



UREMBO wa kuvaa viatu virefu maarufu kama ‘Heels’ umesambaa duniani kote, hata hivyo baadhi ya wanawake wanashindwa kutumia kutokana na ugumu wake.

Kwa mtu anayevaa mara ya kwanza anapata wakati mgumu wakati wa kutembea na asipokuwa makini anaweza kuanguka au kuumia mguu.

Hata hivyo, utapatiwa mafunzo ya namna ya kutumia haitachukua muda mrefu kuanza kuzoea na kisha ukawa miongoni mwa wanawake wanaofurahia urembo huo.

Leo tunawaletea njia sahihi za kujifunza kutembea ukiwa umevaa viatu.

**CHAGUA KINACHOKUTOSHA**

Unatakiwa kuchagua kiatu kinachokutosha vyema, kama vikubwa au vinakubana itakupa shida katika kutembea.

Pia unatakiwa kujua aina ya miguu yako, kuna aina ya viatu kwa wale wenye miguu minene na wenye miguu myembamba haviwakai vizuri.

**ANZA VISIGINO VIFUPI**

Ukitaka kuwa mzoefu wa viatu virefu, lazima uchukue hatua mbalimbali ikiwamo kuanza kuvaa viatu ambavyo vina visigino vifupi, na ukishazoea vaa vyenye urefu kiasi.

**TEMBEA UMBALI MFUPI**

Ukifikia hatua ya kuvaa kiatu kirefu, hakikisha kabla hujatoka navyo matembezi fanya mazoezi kwa kutembea mwendo mfupi ndani kwako.

Unaweza kwenda nacho kazini, lakini hakikisha umebeba viatu vya kawaida kwenye begi lako ili unapoona umechoka unabadilisha.

Hakikisha usianzie umbali mrefu kwani unaweza kushindwa kutembea au ukaanguka na kuumia.

**CHANGAMOTO**

Kuna changamoto mbalimbali zinajitokeza wakati unapoanza kuvaa viatu virefu, ikiwamo maumivu wakati wa kutembea.

Ili kuondoa tatizo hilo unashauriwa wakati wa kutembea uzito uwe kwenye kisigino kwenda kwenye vidole, wengi huwa tunafanya makosa kwa kuweka uzito kwenye vidole kwenda kwenye kisigino na kusababisha maumivu.

MAPISHI

Na Mary Geofrey



# Pilau la njegere







LEO katika safu yetu ya mapishi tunaelekezana namna ya kupika pilau njegere na nyama.

**MAHITAJI**

Pilau masala, mchele kilo moja, chumvi kiasi, mafuta, nyanya, vitunguu maji, vitunguu swaumu vilivyosagwa na tangawizi iliyosagwa.

Binzari nyembamba, supu ya nyama, njegere, nyama nusu kilo, viazi mviringo na maji ya moto.

**MATAYARISHO**

Chemsha nyama ya ng’ombe niliyoiwekea viungo na epua.

Osha mchele kisha acha uchuje maji, weka mafuta ya kutosha kwenye sufuria kisha weka vitunguu maji vikibadilika rangi weka vitunguu swamu na tangawizi baada ya kubadilika rangi weka nyama na kaanga.

Baada ya hapo weka binzari nyembamba na baada ya muda kidogo weka pilau masala, weka viazi mviringo na njegere endelea kukoroga.

Endelea kukoroga mpaka kuiva vizuri ndipo mimina mchele na supu ya nyama ya ng’ombe na malizia na chumvi na ukoroge vizuri na weka njegere.

Funika chakula chako kichemke na kukaukia maji.

Baaba ya kukaukia geuza na kama unapikia mkaa palia na moto juu ya mfuniko.

Tayari chakula chako kitakuwa kimeiva kwa ajili ya kuliwa na kachumbari.

# MAISHA NI NYUMBA



## Dondoo muhimu ya kufanya meza yako ya chakula kupendeza muda wote

**1:** Hakikisha meza ya chakula inakuwa tupu wakati wa muda wa kawaida, weka mapambo ikiwamo maua ili kuongeza mvuto.


**2:** Usiweke vitu vingi kama watu hawapo mezani kwani inaweza kutumika katika shughuli zingine za kifamilia.

**3:** Hakuna umuhimu wa kuweka vitambaa, kwani vitambaa vinatumika wakati wa kula ili mabaki ya chakula isichafue meza.

**4:** Wakati wa kula weka kila kitu muhimu kama sahani, vijiko, upawa, glasi na 'hotpot'za kuhifadhia chakula.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
UMEPOTEZAJE HELA YA NGAMA?
'NGAMA' ATAKUDAI?
JAMANI TUWAELEWEJE? 'NAFASI MOJA YA KAZI' MNAKUJA WATU LAKI MOJA!
KILANGA CHAKO BOSI KWA NINI ULI-TANGAZA!
NYAFASI YA KAZI
HII SIVII KITUKO
MLITUITIA NINI KAMA SIO SHOBO 'MBINUKO?'
WABONGO WAMEZOEA "KUBETI"
NONGWA ZA KISWAZI
KAKA HONGERA NASKIA BINTIYO MWAJEI NTEKENYE UMEMUOZESHA!
SUBIRI KWANZA AFIKISHE MWEZI
BABA MFANYE AWE NA HOFU YA 'KUWAGONGEA' WENZAKE...ENDAPO ATAENDELEA BASI NAE AGONGEWE.. MFULULIZO
AJARIBU MTU AONE!!! WENGINE MILANGO YETU MISONOBALI SIO IMARA
VIBAKULI WAPI TENA WAKATI HUYO JIRANI MKEWE KASAFIRI?
MBONA WEWE MUMEWE AKI-SAFIRI UNA-KWENDAGA KUANGALIA 'SIZONI?'
MUME WANGU NIMEMFUMANIA NYUMBA YA TATU KAJIFANYA YUPO SAFARINI KUMBE ANANISALITI!
'AISEE GOOGLE' HATARI SANA MWENZAKO MIYE WAIFU KANIGUGO' KAJA KUNIFUMA LINDI! NIMEVAA MSULI...JANA!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
MGANGA NAE FUNDI JAPO HATUMII MSUMENO...

## HABARI KIMATAIFA

## Meli ya Iran yaachiwa huru

**TEHRAN,** IRAN

MELI ya mafuta yenye kupeperusha bendera ya Iran, ambayo ilitekwa na Indonesia mapema Januari mwaka huu imeachiwa huru.

Televisheni ya Iran, ilitangaza kuwa meli hiyo imeendelea na safari yake kabla ya kurejea nchini humo.

Serikali ya Indonesia ilisema walinzi wa pwani waliitia nguvuni meli hiyo iitwayo MT Horse, kwa kuishuku kuwa inasafirisha mafuta kinyume cha taratibu katika eneo la bahari la taifa hilo.

Iran ambayo kwa sasa ipo katika vikwazo vya Marekani, kwa mara kadhaa imekuwa ikituhumiwa kufanya mauzo ya mafuta yake kwa kificho.

## Marekani yaiwekea vikwazo Belarus

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imerejesha vikwazo kwa kampuni tisa zinazomilikiwa na serikali ya Belarus.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya taifa hilo kulazimisha kutua kwa ndege ya abiria katika mji mkuu wa Belarus, Minsk ambayo ilikuwa imembeba mwandishi wa habari mpinzani wa serikali ya taifa hilo.

Hata hivyo, taarifa ya Ikulu ya Marekani haijayataja majina ya kampuni zinazokusudiwa.

Pamoja na vikwazo hivyo, serikali ya Rais Joe Baden, inapanga kuongeza orodha ya maofisa wa karibu na Rais Alexander Lukashenko, kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu na rushwa baada ya uchaguzi unaolalamikiwa wa 2020.

Mwandishi huyo Roman Protasevich na mwenzi wake walikamatwa Mei 23, mwaka huu muda mfupi baada ya ndege hiyo kutua katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Minsk na kuibua lawama jumuiya ya kimataifa.

**DW**

# Volcano yalipuka tena DRC

**GOMA,** DRC

MLIPUKO wa pili wa volkano umetokea karibu na mji wa Goma nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) jana.

Wizara ya mawasiliano nchini humo, kupitia ujumbe wa Twitter ilisema mlipuko huo ulikuwa mdogo na ulitokea upande wa kaskazini mwa Nyamulagira.

Ujumbe huo ulisema lava imetiririka kuelekea sehemu ambayo haina makazi ya watu katika Mbuga ya Virunga.

Kabla ya mlipuko huo, maelfu ya watu wanaoishi katika mji wa Goma wanaendelea kuhama kutokana na hofu ya kutokea milipuko mingine ya volkano.

Awali mamlaka za eneo zilisema kulikuwa na hofu kwamba Mlima Nyiragongo unaweza kulipuka tena. Wiki iliyopita mlipuko wa volkano katika mlima wa Nyiragongo ulisababisha vifo vya watu 32, na kuacha maelfu bila makazi, kulingana na taarifa ya Umoja wa Mataifa.

Mlipuko huo mdogo wa jana huenda ukazidisha hofu katika mji huo ambao zaidi ya nusu ya wakaazi wake wameondoka na waliobaki sasa wanatazamia kuchukua hatua kama hzo ili kunusuru maisha yao.

Kabla ya kulipuka tena. Baadhi ya watu walianza kurejea kwenye nyumba zao, licha ya kutolewa onyo kuwapo na tishio ya milipuko mingine ya volcano.

Eneo hilo mpaka jana limepigwa na matetemeko ya ardhi zaidi ya 200 ambayo yamesababisha uharibifu wa majengo na kutokea nyufa mbili ardhini zenye urefu wa mita mia kadhaa.

Gavana wa kijeshi wa jimbo la Kivu Kaskazini, Ndima Kongba, aliamuru kuhamishwa kwa karibu theluthi moja ya wakazi wa mji huo siku ya alhamisi, akisema magma iligunduliwa chini ya Ziwa Kivu lililo karibu na hapo.

"Hivi sasa hatuwezi kuzuia mlipuko kwenye ardhi au chini ya ziwa," Kongba alisema, akiamuru raia wanaoishi kwenye wilaya 10 kuhama.

**BBC**



Wakazi wa mji wa Goma nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wakihama makazi yao baada ya volcano kulipuka kwa mara ya pili katika Mlima Nyiragongo **(PICHA: BBC)**

# Kanali Goita ateuliwa Rais mpya Mali

**BAMAKO,** MALI

MAHAKAMA ya Katiba ya Mali, imemtangaza Kanali Assimi Goita, kuwa rais mpya wa mpito kujaza nafasi iliyoachwa wazi na Rais Bah Ndaw ambaye amejiuzulu. HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/mahakama-ya-mali-yamtangaza-goita-rais-wa-mpito/a-57710416" INCLUDEPICTURE "https://static.dw.com/image/57710308_303.jpg" * MERGEFORMATINET

Katika uamuzi wake, mahakama hiyo ilisema Goita, aliyeongoza mapinduzi ya kijeshi siku ya Jumatatu anapaswa kujaza nafasi hiyo.

Uamuzi huo unazidisha mkwamo wa uongozi, licha ya marais wa mataifa ya Afrika Magharibi wanajiandaa kukutana jana kuzungumzia hatua ya kukabidhi madaraka.

Viongozi hao wanaeleza mgogoro huo unahatarisha harakati za kuelekea kwenye demokrasia na kudhoofisha mapambano dhidi ya wapiganaji wa jihadi katika ukanda huo.

Goita alikuwa makamu wa rais baada ya kuongoza mapinduzi mwezi Agosti mwaka uliopita na kumuondoa madarakani Rais Ibrahim Boubacar Keita.

Ndaw na Waziri Mkuu, Moctar Ouane ambao walishikiliwa baada ya mapinduzi hayo kisha walijiuzulu siku ya jumatano baada ya kushinikizwa na jeshi wakiwa kuzuizini.

Viongozi hao waliokuwa katika serikali ya mpito waliachiwa huru siku moja baadae.

Hayo ni mapinduzi ya pili kufanyika Mali ndani ya kipindi cha mwaka mmoja.

Kanali Goita, ambaye aliwashutumu Ndaw na Ouane kwa kukiuka hati ya makubaliano kuhusu serikali ya mpito na kushindwa kuwasiliana naye kuhusu kufanya mabadiliko ya baraza la mawaziri, ambapo maofisa wawili wa kijeshi walipoteza nafasi zao.

Kiongozi huyo wa kijeshi pia aliwashutumu Ndaw na Ouane, kwa kushindwa kuituliza hali ya mambo nchini Mali, ukiwamo mgomo wa wiki iliyopita ulioandaliwa na shirikisho la vyama vya wafanyakazi.

Hata hivyo, Goita alisema hawakuwa na njia nyingine isipokuwa kuingilia kati.

"Tulilazimika kuchagua kati ya machafuko na mshikamano ndani ya vikosi vya ulinzi na usalama na tulichagua kushikamana," alifanua Goita.

Kanali huyo wa jeshi, alisema atamchagua waziri mkuu ndani ya siku chache zijazo.

Akizungumza kwa mara ya kwanza tangu achukue madaraka, Goita alisema hatua hiyo ilichukuliwa baada ya kufanya mazungumzo na viongozi wa kisiasa na vyama vya kiraia mjini Bamako.

**DW**

**SAFU**

**MAKALA**

# TUSIWAKUMBUKE KWA MAJUTO



Na Magabilo Masambu

> **Wengine watakumbukwa kwa ukali, ucheshi, mizaha kubwa zaidi umuhimu wake katika familia hiyo au ofisini. Kitu kibaya tulichonacho binadamu huwa ni vigumu sana kuona umuhimu wa kitu mpaka kinapopotea.**

BINADAMU tuna utamaduni wa kujenga mazoea. Unapotokea msiba mahala fulani, watu hulia sana juu ya mtu wao wa karibu anapoaga dunia. Wengi wetu hudhani kwamba, kinachotuliza ni juu ya wema wake, lakini nafikiri zaidi tunalia kwa sababu tulizoea kuwa naye, hata kama alikuwa na mabaya kwetu tuliyazoea akiwapo na anapoondoka huruma ya kumkosa hutuingia.

Ukweli kwamba binadamu yeyote anazo pande mbili haupingiki, kwa maana ya uzuri wake ama ubaya wake. Pande hizo ndizo zinazo kamilisha ubinadamu wake, hivyo hatutegemei atapatikana mtu akatenda mazuri tu au mabaya tu bali katika kutenda kwa vyovyote vile kutakuwa na mchanganyiko na hivyo kuleta mgawanyiko wa maoni baina ya mtu na mtu.

Kama ni familia au ofisi inapomkosa mtu ambaye ilimzoea kwa mema yake au mabaya yake, basi baada ya muda fulani mnaweza kujikuta mkimkumbuka ndugu yenu kwa mambo mbalimbali. Wengine watakumbukwa kwa ukali, ucheshi, mizaha kubwa zaidi umuhimu wake katika familia hiyo au ofisini.

Kitu kibaya tulichonacho binadamu huwa ni vigumu sana kuona umuhimu wa kitu mpaka kinapopotea. Mfano, huwezi kuona umuhimu wa njaa ukiwa na shibe, kwahiyo mtu akiwa na njaa utamshangaa, unaweza kuwa na mama kichaa usione umuhimu wake, lakini siku hayupo ndio utajua kwamba hata ule ukichaa wake ulikuwa na maana na sababu yake nimesema ni mazoea.

Unaweza kuwa na mwanamume au mwanamke ukamwita mwanamume suruali au mwanamke gauni, siku hayupo utajua kwamba ulikuwa na suruali, gauni au ulikuwa na mtu muhimu sana katika maisha yako. Wanaume au wanawake ambao wamewahi kuachana na wake au waume zao wa mwanzo, wanaweza kuwa mashuhuda wa hili.

Chochote kinachotokea katika mahusiano mapya ni haraka sana kujaribu kukumbuka mwanzo ulikuwa unaishije na huyo suruali au gauni, si kwamba amefanya maajabu sana kwenye maisha yako, tatizo ni yale mazoea, lakini pia yakitegemea mabadiliko haya mapya, inawezekana kweli ikatokea ukaona kwamba, kwanini ulichelewa kule, lakini bado yapo utakayokuwa unayakumbuka kwasababu kama ulidumu naye kwa muda, kuna mambo uliyapenda, hayo ndiyo yatakufanya umkumbuke.

Tanzania kwa sasa tunaye rais wa sita ambaye anakwenda kukamilisha kipindi cha awamu ya tano ambayo imeishia njiani kutokana na kifo cha Rais John Pombe Joseph Magufuli.

Kwakuwa awamu zinahesabiwa kwa vipindi viwili vyenye jumla ya miaka kumi basi Rais wa sasa Samia Hassan Suluhu anakwenda kuikamilisha awamu ya tano ambayo ingekamilishwa na Rais John Pombe 2025 na wala siyo awamu ya sita kama inavyosemwa na wengi bali tuna rais wa sita katika muhula wa pili wa awamu tano.

Sasa umekuwa utamaduni na ndivyo ilivyo wala haitaanza katika kipindi hiki, kwamba kila tunapopita katika awamu moja kwenda nyingine, kutokana na mazoea tumekuwa hatuoni sana umuhimu wa awamu iliyoko madarakani kwa wakati huo, bali tunakumbuka baadhi ya mambo katika awamu zilizopita.

Ndivyo ilivyo toka awamu ya kwanza, ya mzee Mwinyi, Mkapa, Jakaya, John na hata wakati wa leo wa mama Samia. Tayari yapo mambo ambayo watu wananong'onanong'ona kwamba angekuwepo rais Magufuli hili lisingekuwa hivi na vile wala hawajakosea tatizo ni mazoea. Kwahiyo aliyeko madarakani pia hana sababu ya kuwachukia ni kujaribu kuyatazama yanayofanya mtangulizi wake akumbukwe ili ayarekebishe kupunguza hayo majuto japo nina uhakika hataweza kumridhisha kila mtu.

Sasa hivi kuna maneno huko mtaani na si ya kupuuza yameanza kujitokeza ni muhimu sana kuyatazama, ambayo huko nyuma yalikuwa yameshamiri sana isipokuwa kipindi cha John, tabia ya baadhi wafanyakazi wa umma kutowaheshimu na kuwathamini wananchi katika kuwapatia huduma.

Kuna baadhi ya maeneo yameanza kulalamikiwa, kwamba mbona wakati wa John hayakuwa hivi? Kwa maana ya nidhamu ya watumishi wa umma. Ni muhimu sana kutupia macho maeneo muhimu kama huduma za Polisi, Hospitalini, Mahakama,TRA na ofsi nyinginezo za umma na hasa ambazo huduma zake zinaweza kukaribisha mzungumzo ya rushwa, ili mwananchi kupatiwa huduma.

Hata wakati wa John, kuna baadhi ya maeneo wananchi walitamani kipindi cha Jakaya, kama nilivyosema ni kawaida, lakini muhimu zaidi rais anayekuwa madarakani malalamiko katika eneo fulani, huwa ni taa ya kukuongoza katika kuyarekebisha si rahisi kufanya kama yeye kwasababu ni watu wawili tofauti japo rais wetu alituambia yeye na John ni kitu kimoja.

Ukiachiwa watoto kuwalea una uchaguzi wa mambo mawili, moja kuwafanya wamkumbuke aliyekuwapo kwa kujuta kwamba angekuwepo leo tusingeishi hivi au kuwafanya wamsahau kwa kuyaendeleza yale yanayomfanya wamkumbuke ili kutoona tofauti kubwa sana kati ya mlezi na mzazi wao.

Bahati nzuri ya mlezi ulishaona namna mzazi alivyokuwa akiwalea watoto wake na kama alikuwa anakosea katika kuwalea, utakuwa na nafasi ya kuwabadili fikra kwanza, kwamba hamkupaswa kulelewa hivi malezi mazuri ni haya na baada ya muda watakuwa wamekuelewa na kutokumkumbuka tena badala yake faraja yao inakuwa kwako, lakini ikitokea watu wakamkumbuka baba yao kwa majuto litakuwa jambo baya sana katika maisha yao.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

**BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO**

# Kifo cha Maneti kilivyotikisa nchi



Na Adam Fungamwango

MARIA eeh, Mary. Sikiliza miziki wa Awamu ya Pili Maria, inavyolalamika juu yako. Sina raha Maria, wala Sitamani kula Maria. Kama nasafiri, Tanga Moshi Arusha Sumbawanga, nakufikiria we Maria. Sijapenda namna hii toka kuzaliwa. Na wala sitopenda namna hii toka kuzaliwa. Na wala sitopenda mpaka siku ya kufa. Hahahaha, Maria eee, adios hahahaha."

Hicho ni kipande cha mwanzo cha wimbo wa bendi ya Vijana Jazz uitwao Mary Maria. Ulirekodiwa mwaka 1985 kwenye studio za Radio Tanzania Dar es Salaam.

Hupigwa kwenye vipindi cha muziki, vipindi vya salamu, Wakati wa Kazi, Ombi Lako, na vinginevyo.

Cha ajabu siku hiyo wimbo ulipigwa kwenye kipindi cha Majira. Ni kipindi ambacho wananchi hujuzwa habari mbalimbali za kitaifa zilizotokea nchini Tanzania.

Lakini siku hiyo, kipande cha muziki cha kuashiria kipindi hicho kilipoanza na kumalizika tu, kikafuatia kipande cha wimbo wa 'Mary Maria'.

Ilikuwa ni saa 3:00 usiku, Mei 31 mwaka 1990. Kila aliyekuwa anasikiliza redio alishangaa. Awali ilionekana kana kwamba mtangazaji alichanganya madawa na ataomba radhi kwa hilo. Haikuwa hivyo. Kilipoisha tu sauti ya mtangazaji ilisikika. Ilikuwa ni ya majonzi na huzuni. Ilitamka hivi.

"Mwanamuziki maarufu nchini, mwimbaji na kiongozi wa bendi ya Vijana Jazz, Hemed Maneti amefariki dunia. Maneti alifariki dunia leo saa 11:00 jioni kwenye Hospitali ya Mwananyamala jijini Dar es Salaam alipokuwa amelazwa."

Ilikuwa ni sauti ya mtangazaji Idd Rashid Mchata (marehemu). Wengi hawakuamini. Ni kwa sababu hawakuwahi kusikia kama mwanamuziki huyo mgonjwa.

Ni kweli Maneti alifariki baada ya kuugua kwa muda kidogo, lakini ikumbukwe wakati huo kulikuwa hakuna mitandao ya kijamii kama sasa ya kupenyezeana taarifa za kidaku.

Kesho Mei 31, itakuwa ni siku ya kumbukumbu ya kifo cha mwanamuziki huyo maarufu kabisa kama si nchini, bali Afrika Mashariki, kwani ameshafanya kazi hata nchini Kenya, alipokwenda kurekodi vibao mbalimbali kama 'Masido', 'Stella' na nyinginezo. Pamoja na umaarufu wote aliokuwa nao alifariki akiwa na miaka 37 tu.

Kwa wakazi waliokuwa wakiishi karibu na maeneo ya Hospitali ya Mwananyamala, na vitongoji vyake walipata taarifa ya kifo hicho muda mfupi tu.

Hakukuwa na simu wala mitandao, lakini taarifa tu za mdomo kutoka kwa waliokuwa hospitalini hapo kwa sababu mbalimbali, ikiwemo kuangalia ndugu zao, walisambaza taarifa ambazo zilisababisha umati ujae nje ya geti la hospitali. Wengi waliangua vilio. Walitaka kwenda kuangalia kama ni kweli. Ilibidi ulinzi uongezwe maradufu.

Umati mwingine wa watu ambao ulikuwa mithili ya maandamano, ulianza kukusanyika nyumbani kwake Mtaa wa Kiyungi, Magomeni Morocco karibu kabisa ya Kanisa Katoliki la Magomeni ili kuthibitisha jambo hilo. Hawakukuta msiba.

Ulikuwa ni ndugu yake Salum Faya (marehemu), ambaye aliwahi kuwa kiongozi wa klabu ya Simba.

Yote haya yalitokea kwa sababu wakati huo, Maneti alikuwa mwanamuziki maarufu sana.

Sifa zake, mbali na kuwa kiongozi wa bendi hiyo, lakini utunzi na uimbaji wake, ulisababisha kujizoelea umaarufu na kupendwa na mashabiki wengi wa dansi.

Miezi michache iliyopita alikuwa ametoka kurekodi albamu ya 'Wifi Zangu Mna Mambo', ambayo inasemekana aliirekodi akiwa mgonjwa.

Mbali na hizo, Maneti alitunga na kuimba nyimbo nyingi kama 'Operesheni Maduka', 'Niliruka Ukuta', 'Tambiko la Pambamoto', 'Magaidi wa Msumbiji', "Bujumbura', 'Ngoma', 'Penzi Haligawanyiki', 'Jiko Limenuna', 'Tabu', 'Madaraka kwenye Baa', 'Ogopa Tapeli', 'Charembo', 'Aza Umeniumbua', na nyingine lukuki. Alitunga zaidi ya nyimbo 50.

Alizaliwa Juni 19, 1954 kijiji cha Mamboleo, Bombuera Silas Estate, Muheza mkoani Tanga, wazazi wake wakiwa wahamiaji kutokea Sumbawanga mkoani Rukwa, wakifika huko kwa ajili ya kazi za mashamba ya mikonge.

Muziki aliuanza alipokwenda kumtembea dada yake mjini Morogoro. Alimueleza dada yake azma ya yeye kutaka kuwa mwanamuziki, kutokana na dada yake huyo kufahamiana na gwiji la muziki mkoani hapo, Juma Kilaza. Dada alimuombea na alikwenda kufayiwa marajiribio akafaulu. Ndipo alipojiunga na Cuban Marimba na kutunga nyimbo nyingi ikiwemo 'Subisubi'. Baadaye yeye na Kilaza waliunda bendi ya TK Limpompo na kutunga nyimbo kama 'Maisha ya Sasa', kabla ya kujiunga na Vijana Jazz mwaka 1974. Alizikwa Juni 2 kijijini kwao Mamboleo.

Pamoja na muziki, hadi anafariki Maneti pia alikuwa Mwenyekiti wa UVCCM Ndugumbi, tawi la Magomeni na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Vijana Taifa.

Kesho itatimia miaka miaka 31 kamili, akiwa amelala chini ya tumbo la ardhi, lakini kazi aliyoiacha duniani bado itaendelea kukumbukwa na kuwa burudani kwa vizazi na vizazi.

# HADITHI

MILIO mitatu ya risasi ilisikika maeneo ya Keko Bora, Dar es Salaam. Sauti hizo za risasi ziliwafanya watu kutimua mbio na kutafuta chaka la kujificha. Kila mmoja alidhani ni majambazi waliovamia kwa ajili ya kupora pesa dukani au kwenye vibanda vya mawakala wa kampuni za simu.Haikuwa hivyo. Aliyedhaniwa kuwa ni jambazi alichofanya ni kumpora mwanamke mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja tu na kuondoka naye akiwa kwenye gari aina ya Toyota IST. Huyu jamaa aliyefanya hivyo ni nani? Ni kwa nini alimteka mtoto? Mtoto ni wa nani? Mwanamke aliyeporwa mtoto anamfahamu mporaji? Fuatilia kisa hiki kitamu, cha kusisimua na kuhuzunisha.

# Sumu ya mapenzi-8

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

WALA haikuwa kazi kubwa sana kwa Said. Jumamosi ya kwanza tu alifanikiwa.

Ilirahisishwa zaidi alipoletwa na Doris mwenyewe na kuonyeshwa geti ambalo anayetakiwa kufuatiliwa atatoka. Akapewa na picha, na gari analopenda kutumia.

Saa nne asubuhi geti lilifunguliwa na Said aliiona gari ambalo aliambiwa jamaa anapenda kutumia. Alipoangalia picha aliyopewa haikutofautiana na sura ya mwenyewe.

Aliwasha bodaboda yake na kulifuatia nyuma kwa uangalifu. Mwisho wa safari ulikuwa ni kwenye nyumba moja Magomeni Mikumi, karibu kabisa na kwenye kiwanda cha kutengeneza tambi.

Alisimama kwa mbali kidogo. Ndipo alipomuona jamaa akiteremka peke yake. Lakini baada ya dakika kadhaa alifika msichana mmoja ambaye alikumbatiana na jamaa huyo, wanapigana mabusu, wakashikana mikono kuingia ndani.

Kwa sababu alidokezwa kidogo sababu, Said kwa kujiongeza alichukua picha fupi ya video, na picha tatu za mnato.

"Picha zao hizi hapa." Alimuonyesha. Alizichukua picha zote zile na kuweka kwenye simu yake ili iwe ushahidi baadaye itakapohitajika.

Baada ya dakika tano za ukimya, akiwaza hili na hili, Doris alijikuta akisema "Ananitambua huyu."

"Nani sasa huyu demu au jamaa yako?" Said alimuuliza.

"Wewe kazi yako imekwisha, pesa yako hii, ahsante sana." Doris alimjibu.

"Lazima nidili nalo hizi, vinginevyo nitampoteza Donald." Alijiambia mwenyewe.

Hata hivyo, bado hakujua nini afanye. Alijipa muda kwanza kichwa chake kitulie, aone hatua gani za kuchukua. Na ni zipi? Azifanye peke yake asimwambie mtu yeyote? Awaambie wazazi wake pekee. Au awashirikishe pia wazazi wa Donald? "Muda utaongea." Alipanda kwenye gari yake kutoka pale alipokutana na Said, kurudi nyumbani kwake, Ununio.




**Alipomtazama tu aligundua kuwa ni mwanamke mwenye uwezo. Inawezekana pia na madaraka. Alikuwa ameshika ufunguo wa gari. Mita chache kutoka pale kulikuwa na gari imepaki. Wala hakujiuliza mara mbili kuwa gari hilo ndilo alilokuja nalo mgeni.**

**********************

"Hodi wenyewe." Sauti ilisikika nje ya mlango mkubwa.

Mtu mmoja aliufungua.

"Habari za hapa."

"Nzuri, samahani. Namuulizia dada mmoja anaitwa Tausi."

"Tausiii..." Aliitwa na kijana aliyefungua mlango.

Dakika moja baadaye alisimama mlangoni msichana aliyekuwa amevaa kijora.

Tausi alimuangalia mgeni wake, lakini hakuweza kumtambua. Alikuwa anamuona kwa mara ya kwanza.

Alipomtazama tu aligundua kuwa ni mwanamke mwenye uwezo. Inawezekana pia na madaraka. Alikuwa ameshika ufunguo wa gari. Mita chache kutoka pale kulikuwa na gari imepaki.

Wala hakujiuliza mara mbili kuwa gari hilo ndilo alilokuja nalo mgeni.

Kwa mbali alianza kuwa na wasiwasi. Hakuwahi kupokea mgeni yeyote wa aina hiyo. Hasa wa kike.

Rafiki zake ni hawa hawa tu wa kuja kukopeshana blauzi, madela, vijora, mawigi, manukato na kudaiana.

Alishindwa hata kumkaribisha mgeni. Alibaki amesimama huku miguu ikiwa kama ina ganzi.

"Habari yako dada."

"Nzuri, karibu."

"Ahsante, samahani wewe ndiye Tausi?"

Alisita kidogo, lakini kiu ya kutaka kujua kitu gani kinaendelea alijikuta akijibu "Ndiyo?"

"Ooh, vizuri sana, nimefurahi kukufahamu."

Tausi aliendelea kuvurugwa. Wakati mgeni wake akishukuru kumfahamu, yeye bado hajamfahamu mgeni wake.

"Naomba tutete kwanza. Nina salamu zako."

"Salamu gani?"

"Tausi, mimi naitwa Doroth. Ni mchumba wa Donald. Nataka kumwambia kitu. Wewe ni mwanamke mwenzangu. Achana na Donald. Niachie Donald wangu."

Maneno hayo yalifanya tumbo la Tausi kushtuka na kuanza kuuma ghafla. Alianza kujisikia vibaya, tumbo likikata. Lakini alijikaza.

"Wewe dada we. Mbona unaniletea habari ambazo mimi sizijui? Donald mchumba wako, halafu mimi nahusika vipi hapo?"

"Tausi, najua kila kitu. Mimi si mtoto mdogo. Nimewafuatilia siku nyingi. Nimegundua kuwa unatembea na mchumba wangu. Tunataka kufunga ndoa. Lakini wewe imeliingilia penzi langu."

"Eeeh, jamani, makubwa haya. We dada mbona mi sikuelewi?"

"Nisikie mdogo wangu. Mimi sikuja kwa shari. Ningekuwa mshari nisingekuja kukwambia. Ningefanya ninachotaka kufanya, lakini nimekuja kukwambia tu kwa upendo tu."

"Sasa ndiyo nakwambia mimi huyo mchumba wako simjui. Na wewe ulipaswa umkalishe huyo mchumba wako chini umwambie atulie nyumbani, sijui umfunge kamba asitembee. Wee kiguu na njia hadi huku, mimi nahusika vipi hapo kama siyo kutafutana muhali?" Tausi aliongea akiwa ameshika kiuno, huku akijitikisatikisa, akimuangalia mgeni wake kuanzia chini hadi juu.

"We ninyali tu, unajua mimi siyo mtoto wa uswahilini. Ila nachokwambia kifanyie kazi, usije ukaniona mimi mbaya." Doroth alisema huku akipiga hatua kwenda kwenye gari lake. Kwanza aliona mzozo umeanza kuwa mkubwa, huku watu wa uswahilini wakiwa hawana dogo. Wameshaanza kujaa. Kingine hakumuweza Tausi kwa kuongea. Yeye mtoto wa ushuani, mwenzake wa uswazi. Neno moja mwenzake kumi. Hiyo ilizidisha hasira, hivyo aliona anaweza kufanya kitu ambacho atakuja kujuta baadaye. Sababu nyingine ni kwamba kazi iliyompeleka alishaitekeleza. Kumfahamisha kuwa Donald ana mchumba. Kama alikuwa anamdanganya basi ajue hivyo. Mwisho ni kumpiga mkwara.

Hakupata tabu sana kupafahamu kwa kina Tausi. Aliletwa na Said jamaa wa bodaboda hadi kwenye nyumba ya kina Sadiki. Hakumfahamu jina, ila aliuza kuwa anamuulizia msichana mmoja, akataja wajihi wake ambao aliuona kwenye picha ya video iliyopigwa na Said, akiwa na Donald, ndipo walipomwambia kuwa msichana anayemtafuta anaitwa Tausi, lakini hakai hapo. Akaelekezwa nyumbani kwao.

"Wanawake wengine bwana. hovyoo. Yaani mchumba ndiyo unanifuata kunipiga mkwara, angekuwa mume je?" Bado Tausi alizidi kumsindikiza Doroth na maneno ambayo hayo hakuyasikia, kwani gari lake lilishaanza kuondoka akiwa ameshafunga vioo.

**INAENDELEA JUMAPILI**



# TUZO ZA OSCAR ZASOGEZWA MBELE

IMESHTUA! Ni kama Dunia imesimama ghafla baada ya sherehe za utoaji wa Tuzo za Oscars, kuahirishwa na kusogezwa mbele hadi Machi 17, mwaka 2022.

Awali utoaji tuzo hizo ulipangwa kufanyika Februari 27, mwakani, lakini kutokana na sababu za kusambaa virusi vya corona, kamati inayosimamia sherehe hizo imeamua kusogeza mbele.

Ratiba mpya imetoka jana inaonyesha matukio yote yaliyopangwa kufanyika kwenye ukumbi wa Dolby Theatre huko Hollywood & Highland Center nchini Marekani.

Tuzo za Oscar hufanyika kila mwaka na kampuni ya Academy of Motion Picture Arts and Sciences (AMPAS) kwa lengo la kutambua mchango wa taaluma ya tasnia ya filamu, wakiwamo waongozaji, waigizaji, na watunzi wa filamu.

## Kiba asababisha moto Kenya

WAKENYA wamewavuruga tena Watanzania baada ya mwanamuziki Ali Kiba, kulalamika amezushiwa uongo kwa kuambiwa ana watoto saba.

Tukio hilo lilianza baada ya Blog moja nchini humo kuandika msanii huyo anatarajia kupata mtoto wa saba muda wowote, ndipo Kiba kupitia akaunti yake ya Twitter, aliandika kuwa ni uongo.

Muda mfupi baada ya kuandika neno hilo, mashabiki wake walivamia mtandao huo na kuanza kushambulia kwa maneno makali.




## Barnaba we mkali bhana

MASHABIKI wa muziki wa Bongo Fleva nchini, wamezidi kupagawishwa na wimbo mpya wa Barnaba unaitwa 'Cheketua' kutokana na mistari yake inayowavutia warembo.

Kwa ujumla Barnaba akishirikiana na Ali KIba, umekuwa ukitamba kila kona na wengi wa wasikilizaji wanasema ndani yake kuna utajiri wa misemo ya Kiswahili.

Naupenda wimbo huu jamani, ukiwasikiliza barnaba na Ali Kiba wamejitahidi kuweka misemo ya Kiswahili na yenye kumvutia kila mtu," amesema Amina Saidi.



# Nike yataja sababu kumtema Neymar

**LOS ANGELES,** Marekani

KAMPUNI ya vifaa vya michezo ya nchini Marekani, Nike, inasema iliacha kufanya kazi na mwanasoka wa Brazil, Neymar kwa sababu "alikataa kushirikiana katika uchunguzi kwa nia njema" juu ya madai ya unyanyasaji wa kingono dhidi ya mfanyakazi.

Tukio hilo linadaiwa lilitokea mnamo mwaka 2016 na kuripotiwa kwa Nike mwaka 2018.

Msemaji wa Neymar, alisema alikataa unyanyasaji wa kijinsia na akajitenga na Nike mwaka jana kwa sababu za kibiashara.

Nike iliachana na Neymar Agosti 2020, na kumaliza moja ya mikataba yake ya udhamini wa hali ya juu na kampuni hiyo haikutoa sababu ya kutengana naye wakati huo.

Katika taarifa yake ya juzi Nike ilisema: "Haitakuwa sahihi kwa Nike kutoa taarifa ya mashtaka bila kuweza kutoa ushahidi wa kuunga mkono."

Lakini iliongeza: "Nike ilimaliza uhusiano wake na mchezaji huyo kwa sababu alikataa kushirikiana katika uchunguzi kwa nia njema kuhusu madai ya kumdhulumu mfanyakazi."




# LINGARD YUPO TAYARI KURUDI WEST HAM




**LONDON,** England

JESSE Lingard amewaaga wachezaji wenzake kupitia kurasa zake za mitandao ya kijamii, lakini hajaweka kizuizi juu ya uwezekano wake wa kurejea tena West Ham kwa siku zijazo.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, alifanya vema sana akiwa na klabu hiyo ya London Mashariki tangu alipojiunga nayo akitokea Manchester United Januari, mwaka huu.

Lingard amefanikiwa kufunga mara tisa, na kutoa pasi za mwisho tano kwenye mechi 16 alizocheza Ligi Kuu England, akiwa na mchango wake kwenye klabu hiyo kufuzu kucheza Ligi ya Europa msimu ujao.

Lingard akizungumzia namna bora ya kumaliza msimu kwenye chapisho lake, amesema yeye pamoja na kikosi chake hapo West Ham wamefanikiwa kufikia lengo ambalo walijiwekea.

"Haijalishi kesho itakuwaje, lakini West Ham itakuwa na nafasi ya pekee sana kwenye moyo wangu," alisema Lingard akinukuliwa na BT Sport.

Lingard amebainisha kuwa klabu imempa nafasi ya pekee ya kurejesha ubora wake baada ya kutoka Man United.

Pia amewashukuru mashabiki kwa kumsapoti tangu alipowasili kwa 'Wagonga Nyundo' hao wa jijini London.

# *Griezmann, Coutinho wanukia panga Barca*

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, yupo tayari kupitisha panga kwenye kikosi cha kwanza cha miamba hiyo ya Nou Camp kusafisha wachezaji wasiohitajika na kuleta wengine wapya.

Antoine Griezmann na Philippe Coutinho ni miongoni mwa wachezaji wanaotajwa wanaweza kuwamo kwenye orodha hiyo ya watakaopigwa bei dirisha hili la uhamisho wa majira ya joto.

Kutupwa nje mapema kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kushindwa kubeba ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, umewafanya Barcelona kuja na mkakati wa kubadili kikosi chao.

Kwa mujibu wa BT Sport, kwa kuanzia watahakikisha Lionel Messi anapewa mkataba mpya.

Mabosi wa Barcelona wana uhakika mkubwa Messi atasaini mkataba mpya, huku jambo hilo likiwafanya wafungue milango ya kutokea kwa nyota wengine.

Wachezaji wengine wanaotajwa huenda wakaondoka ni Ousmane Dembele, Miralem Pjanic, Martin Braithwaite, Junior Firpo na Neto.

Beki wa kati, Samuel Umtiti, naye anaweza akaondoka kutokana na kusumbuliwa na majeruhi ya mara kwa mara.

Matheus Fernandes naye yupo kwenye orodha ya watakaouzwa huku Riqui Puig akijiandaa kutolewa kwa mkopo.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AWAAGA WACHEZAJI JUVENTUS

●●● Mkataba wa mchezaji huyo unamalizika Juni 2022, lakini anaweza kuondoka majira haya...

**TURIN,** Italia

CRISTIANO Ronaldo ameripotiwa kuwaambia wachezaji wenzake wa Juventus kwamba anatarajia kuondoka klabuni hapo msimu huu wa majira ya joto.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Real Madrid, aliwasili Turin kutoka mji mkuu wa Hispania Madrid mwaka 2018, lakini ameona msimu ukipita bila ubingwa wa Serie A.

Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, hapo katika dimba la Allianz unamalizika Juni 2022, ingawa anaweza kuondoka Juve msimu huu wa majira joto.

**Kwa mujibu wa Il Messaggero, Ronaldo amewaambia wachezaji wenzake wa Juventus kwamba anataka kuondoka katika dirisha hili la uhamisho.**

Nyota huyo wa kimataifa wa Ureno ameripotiwa kuwaambia wachezaji wenzake hao kwamba, ataondoka mara baada ya michuano ya Euro 2020 inayoanza mwezi ujao.

Manchester United na Sporting CP wamehusishwa na kumtaka tena nyota wao wa zamani baada ya Real Madrid kukataa nafasi ya kumsajili tena. Pia miamba ya Ligi Kuu Ufaransa, PSG nayo imetajwa kuwania saini ya mchezaji huyo.

Katika miaka yake mitatu pale Turin, Ronaldo amefunga mabao 101 na kutoa pasi za mwisho 22 katika mashindano yote kwa 'Bianconeri' hao.

## ZISIKUPITE

### STERLING SASA KUUZWA

MANCHESTER City inajiandaa kumuuza mshambuliaji wake, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 26 kipindi hiki cha majira ya joto baada ya kukaa hapo kwa miaka sita. ***(Mail)***

### HAALAND ATOA NENO

NYOTA wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20, amesema anaheshimu mkataba wake na timu yake, licha ya kuhusishwa na mpango wa kuondoka. ***(Viaplay, via Independent)***

### BARCA WAJIPA MATUMAINI

BARCELONA wanajiamini kwamba watakamilisha usajili wa mshambuliaji wa Manchester City, Sergio Aguero mwenye umri wa miaka 32, na mlinzi wa Uholanzi, Georginio Wijnaldum, 30. ***(Sky Sports)***

### POGBA KURUDI JUVE

KIUNGO wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28, anataka kurudi tena Juventus. ***(Calciomercato)***

### TUCHEL KUJIFUNGA CHELSEA

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, yupo tayari kuongeza muda zaidi wa kukaa kwa Blues hao. Tuchel mwenye umri wa miaka 47 raia wa Ujerumani, mkataba wake wa sasa ni wa mwaka mmoja. ***(Telegraph)***

### LIVERPOOL KUUZA NYOTA NANE

LIVERPOOL inaweza kuingiza kiasi cha pauni milioni 80 kama itawauza wachezaji wake nane wakati wa dirisha la usajili akiwamo winga wa Uswisi, Xherdan Shaqiri mwenye umri wa miaka 29, straika wa Ubelgiji, Divock Origi, 26, na Takumi Minamino mwenye miaka 26. ***(Liverpool Echo)***

### OSCAR ATAKA KURUDI CHELSEA

KIUNGO wa zamani wa Chelsea, Oscar, mwenye umri wa miaka 29, anataka kurudi Stamford Bridge, ikiwa ni miaka minne tangu nyota huyo wa Brazil alipoondoka na kwenda China kujiunga na timu ya Shanghai Port. ***(Goal)***

### BERGWIJN ATAKIWA AJAX

AJAX inawania kumsajili winga wa Tottenham Hotspur na Uholanzi, Steven Bergwijn mwenye umri wa miaka 23. ***(De Telegraaf)***

### VARANE HATAKI MADRID

MLINZI wa kati wa Real Madrid, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 28, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United, amesisitiza hana mpango wa kuondoka. ***(Mail)***

### BALBUENA HURU KUONDOKA

WEST Ham United imemuambia mlinzi wa kati raia wa Paraguay, Fabian Balbuena mwenye umri wa miaka 29, yupo huru kutafuta klabu nyingine mkataba wake utakapomalizika. ***(Football Insider)***

## Mafunzo yavutwa shati ubingwa Z'bar

**Na Hawa Abdallah Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Mafunzo imepunguzwa kasi ya kuukaaribia ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya juzi kupokea kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Mlandege .

Bao pekee la Mlandege lilodumu kwa dakika zote 90 lilifungwa na mkongwe wa timu hiyo, Sabri China katika dakika ya 36 mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Mau A Visiwani hapa.

Mafunzo ambayo kama ingepata alama tatu katika mchezo huo ingeendeleza mbio zao za ubingwa kwa kuwa nyuma ya alama mbili dhidi ya vinara wa ligi hiyo, KMKM yenye alama 37, sasa inaendelea kubaki nafasi ya pili na kwa alama zake 32 baada ya kupoteza mechi hiyo.

Kwa upande wa Mlandege nao wanatakiwa kuhakikisha sasa wanashinda michezo miwili na kuwaombea mabaya ya kufungwa wapinzani wao ambao wapo juu yao katika msimamo wa ligi ili timu hiyo ibaki katika Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao.

## Soka Ufukweni wapata darasa

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Tazania ya Soka la Ufukweni, imetupwa nje kwenye Fainali za Afrika za michuano hiyo (SBAFCON) baada ya juzi kukubali kipigo cha mabao 4-2 dhidi Misri katika mchezo wa kuwania nafasi ya tano.

Mchezo huo Tanzania dhidi ya Misri wa kuwania nafasi ya tano, ulipigwa katika Ufukwe wa Sally, pembezoni mwa Bahari ya Atlantic jijini Dakar, Senegal zinapofanyika fainali hizo.

Tanzania imekamilisha mechi zake za michuano hiyo bila kushinda hata mchezo mmoja kutokana na kufungwa mabao 4-3 dhidi ya Uganda, 3-1 dhidi ya wenyeji Senegal kwenye Kundi A.

Akizungumza na gazeti hili jana, nahodha wa timu ya Tanzania ya Soka la Ufukweni, Jaraf Rajab, alisema mashindano yalikuwa na ushindani mkubwa na wamepata cha kujifunza licha ya kutolewa kwenye michuano hiyo.

# MWAKINYO ATWAA MKANDA ABU WA AFRIKA, JONGO CHALI

**Na Mwandishi wetu**

WAKATI bondia Hassan Mwakinyo akifanikiwa kutwaa ubingwa wa Afrika (ABU) wa uzito wa Super Welter kwa kushinda kwa knockout (KO) dhidi ya mpinzani wake Antonio Mayala, bondia Jongo Shaaban, amewaangusha mashabiki wake baada kupigwa kwa KO dhidi ya Mnigeria Olanrewaju Durodora.

**Mwakinyo ametwaa ubingwa huo Ijumaa usiku katika raundi ya tisa kwenye Ukumbi wa Next Door Arena, Dar es Salaam kwenye pambano kali na la kusisimua lililoandaliwa na Kampuni ya Jackson Group chini ya Ofisa Mtendaji Mkuu, Kelvin Twissa**

Bondia huyo alikabidhiwa mkanda wa ubingwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Damas Ndumbaro sambamba na Waziri wa Michezo, Innocent Bashungwa na Mkurugenzi wa Maendeleo ya michezo, Yusuph Singo.

Mbali ya viongozi hao, katika makabidhiano hayo pia walikuwapo Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya KCB, Cosmas Kimaro, Mkurugenzi wa Multichoice Tanzania, Jackline Woiso na Meneja Masoko wa M-Bet Tanzania, Allen Mushi.

Mwakinyo hakupata ushindi huo kirahisi kutokana na Mayala kupigana kwa mbinu kubwa huku akitegua mitego kadhaa.

Mayala aliingia raundi ya tisa kwa 'pupa' kwa kujua kuwa Mwakinyo amechoka, jambo ambalo lilimponza na kudumu kwenye raundi hiyo kwa sekunde 55 tu, baada ya kupigwa konde kali la mkono wa kushoto na kwenda chini moja kwa moja na kushindwa kuendelea na pambano.

Baada ya kuibuka kidedea, Mwakinyo alisema: "Namshukuru Mungu kwa ushindi huu, natamani kufika mbali zaidi na kupigana na mabondia wakali zaidi duniani, na niliahidi kutowaangusha Watanzania na Rais Mama Samia Suluhu Hassan," alisema Mwakinyo.

Wakati huo huo bondia aliyepewa nafasi kubwa ya kushinda ubingwa wa ABU wa uzito wa juu, Shaaban Jongo alichapwa kwa KO na bondia Olanrewaju Durodora wa Nigeria katika raundi ya pili.

Jongo alitawala sana pambano hilo, ila alijikuta anachezea kichapo baada ya kutojilinda na kupigwa ngumi kali kutoka kwa Mnigeria huyo na kushindwa kuendelea katika pambano hilo lilillodhaminiwa na Benki ya KCB, Bodi ya Utalii, DStv, Onomo Hotel, M- Bet, Plus Networks Limited.

Pia bondia Ibrahim Class, alishinda kwa pointi mpinzani wake, Sibusiso Zingane wa Afrika Kusini huku bondia Hamis Palasungulu akichapwa kwa KO na Ardi Ndembo wa Congo Brazzaville katika pambano la uzito wa juu.

Naye bondia Imani Daudi akishindwa kwa pointi dhidi ya Chris Thompson na Leila Yazidu akipoteza kwa pointi dhidi ya bondia kutoka Bulgaria, Joana Nwamerue. Pia Daniel Matefu alichapwa kwa pointi na bondia wa Bulgaria Pencho Tsvetkov.




Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), Abdallah Bulembo, akizungumza na waadishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kulitaka shirikisho hilo kubadilisha katiba kabla ya uchanguzi mkuu kufanyika Agosti 7, mwaka huu. **PICHA:**

# Azam yaiweka kando Simba, akili sasa Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

HUKU Tanzania ikiwa na uhakika sasa wa kuingiza timu nne msimu ujao kwenye michuano ya kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), uongozi wa Azam FC, umeweka kando mechi ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) dhidi ya Simba na kuelekeza nguvu zote Ligi Kuu Bara kuelekea mechi yao dhidi ya Gwambina FC.

Kutokana na Simba kufanya vizuri kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu, Tanzania sasa ni miongoni mwa timu 12 barani Afrika ambazo zitapata nafasi msimu ujao wa kuingiza timu nne kwenye michuano hiyo ya CAF, mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho Afrika.

Hata hivyo, kulingana na kanuni za Shirikisho la Soka nchini (TFF), bingwa wa Ligi Kuu huiwakilisha nchi michuano ya Ligi ya Mabingwa huku timu itakayobeba Kombe la ASFC (FA Cup) ikipewa jukumu la kuipeperusha bendera nchini Kombe la Shirikisho Afrika.

Lakini kutokana na uwapo wa nafasi hizo nne, ni wazi sasa timu itakayomaliza nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu Bara itakata tiketi ya kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa, huku itakayoshika nafasi ya tatu nayo ikipeperusha bendera ya nchi kimataifa kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, alisema wanahitaji kushinda mechi zilizopo mbele yao iwe wanacheza nyumbani au ugenini ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kumaliza kwenye nafasi ya pili ya ligi hiyo.

Alisema wanachokifikiria sasa ni jinsi ya kujiandaa kwa mchezo dhidi ya Gwambina ambao wanaamini utakuwa mgumu kutokana na ushindani uliopo, na baada ya hapo ndipo watageuzi akili zao kwenye maandalizi ya nusu fainali ya ASFC.

"Hatuwezi kufirikia mchezo wetu wa Juni 24 dhidi ya Simba kwani kabla ya nusu fainali hiyo tuna kibarua cha ligi dhidi ya Gwambana FC, mechi itakuwa ngumu na ushindani mkubwa kwa sababu tunahitaji pointi tatu kwenye mchezo huo ili tuendelee kujiweka sawa katika malengo yetu ya kumaliza ligi tukiwa nafasi ya pili," alisema Vivier.

Alisema baada ya kupata pointi tatu muhimu katika mchezo huo watarejea uwanjani kufanyia kazi upungufu na ubora wa Simba kuelekea mchezo huo wa nusu fainali ya ASFC ambao nao ni muhimu kwao pia kuhakikisha wanacheza fainali na kutwaa kombe hilo.

"Hakuna mechi ambazo si muhimu kwetu, sasa hivi tunahitaji kupata ushindi katika ligi ili kufikia malengo hayo, lakini pia tunahitaji kucheza fainali ya ASFC lazima tupambane nayo tushinde dhidi ya Simba," alisema kocha huyo.

Alisema wamebakiza michezo minne ambayo miwili wanacheza nyumbani ikiwamo dhidi ya Gwambina na Simba na ugenini dhidi ya Mwadui FC na Ruvu Shooting ambazo wanahitaji kukusanya pointi 12 katika michezo hiyo.

Kikosi cha Azam FC kitaingia kambini kesho kujiandaa na mchezo huo dhidi ya Gwambina FC, utakaopigwa Juni 18, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Dar es Salaam.

Michezo
Jumapili Mei 30 , 2021
Nipashe




Ronaldo awaaga wachezaji Juve UKURASA 22

KWA KO...




Waziri wa Maliasili na Utalii, Damas Ndumbaro (wa nne kulia), akimvisha mkanda wa uzito wa Super Welter wa Afrika, bondia Hassan Mwakinyo baada ya kumtwanga Muangola Antonio Mayala kwa KO katika raundi ya tisa kwenye pambano la kuwania ubingwa wa ABU lililofanyika kwenye Ukumbi wa Next Door Arena, Dar es Salaam juzi usiku. Wanaoshuhudia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya KCB, Cosmas Kimaro (wa tatu kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa MultiChoice, Jakline Woiso (wa tatu kushoto) na CEO wa Jackson Group Sports, Kelvin Twissa (wa pili kushoto). **NA MPIGAPICHA WETU**

# Simba yabaki mawinguni, Morrison atupia la mwaka

## ●●● Kwa matokeo hayo sasa imefikisha pointi 64 huku ikiwa nyuma michezo mitatu.....

**Na Adam Fungamwango**

DAKIKA 12 tu kabla ya mechi kumalizika jana zilitosha kwa Simba kufunga mabao matatu na kuiwezesha kuondoka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Namungo FC, kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, hivyo kuendelea kupepea mawinguni kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara.

**Wakati huo Simba ilikuwa nyuma kwa bao 1-0 na ilionekana kama inakwenda kupoteza mechi hiyo, kabla ya kuanza kufungua ukurasa wa mabao kuanzia dakika ya 78.**

Simba ilionekana kubadilika na kufanya mashambulizi mfululizo baada ya kuingia kwa wachezaji watatu, nahodha John Bocco aliyefunga bao la pili na Bernard Morrison aliyefunga bao la tatu na Hassan Dilunga aliyewachachafya vilivyo mabeki wa Namungo FC, wakichukua nafasi za Rally Bwalya, Mzamiru Yassin na Meddie Kagere.

Hakuna timu yoyote iliyofanya shambulizi la hatari kwa dakika 20 za mwanzo. Shambulizi la kwanza la ghafla lililofanywa dakika ya 21 na Namungo FC liliwapatia bao lililotiwa ndani ya nyavu na Mrundi Styve Nziogamasabo aliyeitendea haki pasi ya Talients Lusajo baada ya kumzunguka Pachal Wawa na kumzidi mbio, kabla ya kumpasia mfungaji.

Baada ya hapo ndipo Simba ilipoonekana kama inataka bao na dakika ya 27, Kagere aliachia shuti kali lililopaa juu ya lango.

Kipa Jonathan Nahimana aliifanya Namungo FC kuwa salama dakika ya 40, baada ya kuokoa mara mbili mfululizo shuti la Chris Mugalu, akizuia na mguu, ukamrudia tena mchezaji huyo akaruka juu na kupiga kichwa, lakini ukaokolewa tena kwa ustadi na kipa huyo.

Mugalu tena alikosa bao baada ya kupiga kichwa cha mbizi dakika moja kabla ya mapumziko, kufuatia krosi ya Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr'.

Kipindi cha pili hasa mwanzoni Namungo FC iliendelea kuibana Simba na kuwafanya wachezaji wake kupoteza mwelekeo.

Ndipo zilipofika dakika 12 za furaha kwa Wanamsimbazi hao pale Mugalu aliposawazisha bao, akiunganisha krosi kutoka kwa Shomari Kapombe dakika ya 78.

Ilionekana kama mechi hiyo ingekwenda sare, lakini krosi ya Mugalu dakika ya 83, ilitua kichwani kwa nahodha Bocco aliyeukwamisha wavuni na kuamsha hoi hoi kwa mashabiki wa Simba ambao kwa muda mrefu walikuwa kimya.

Wakati wachezaji wa Namungo wakiwa wamecharuka kusaka bao la kusawazisha, Morrison akiwa katika mstari wa dura la katikati ya uwanja, alimchungulia Nahimana na kubaini kasogea mbele kidogo kisha akaachia shuti la mbali la kushtukiza, lililokwenda moja kwa moja wavuni, huku kipa huyo ayejaribu kuufuata mpira huo bila mafanikio, akiishia kuanguka chini na mpira kujaa kambani.

Kwa matokeo hayo, Simba imefikisha jumla ya pointi 64 huku ikiwa mechi tatu nyuma ya Yanga inayoshika nafasi ya pili na alama zake 61 baada ya kushuka dimbani mara 29.

## Mwakinyo bingwa ABU, Jongo chali

**Na Mwandishi wetu**

WAKATI bondia Hassan Mwakinyo akifanikiwa kutwaa ubingwa wa Afrika (ABU) wa uzito wa Super Welter kwa kushinda...

HABARI UK. 23

## Griezmann, Coutinho kukatwa Barca




**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, yupo tayari kupitisha panga kwenye kikosi cha kwanza...

HABARI UK. 21

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >